



Aibu Afrika kusujudia Ulaya, Marekani – Profesa Uk. 12

Mwabukusi atikisa mdahalo TLS

“Hatuwezi kuwa na wakilishi-ambaye dereva wake ana sifa kubwa kuliko mbunge, hizi sifa za kusoma na kuandika hazilisaidii Bunge kuisimamia serikali...”

Soma zaidi Uk. 4



Soma Ndani

Tibaijuka akemea ‘uchawa’ ni angamizo

Soma Uk. 30

Watoto wa kiume Tanzania hatarini

Na Mwandishi WETU

HALI sasa imebadilika. Watoto wa kiume wamebainika kuwa ndiyo wanaonyanyaswa zaidi kingono kuliko wasichana wadogo.

Wanaozungumzwa hapa ni watoto wa kiume wenye umri kuanzia mwaka mmo-

Soma Uk. 18

Ndani


Safu kamambe

- Askofu Bagonza
- Dkt. Kijo Bisimba
- Evarist Chahali
- Jicho la Tai

TRC yalichafua Pambazuko, mhariri ang’aka

● Ataka majibu ya maswali 12

soma Uk 15



Tahariri/Katuni

Ulega, shirikiana nasi upate majina ya wezi mnadani

JUMANNE ya Julai 16, 2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kupitia kitengo chake cha mawasiliano, ilitoa taarifa kwa umma, ikituhumu gazeti la Pambazuko – Namba 079, toleo lake la Julai 8, mwaka huu kwamba lilipotosha habari kuhusu ufisadi kwenye Mnada wa Mifugo wa Kimataifa wa Pugu.

Katika taarifa hiyo kwa umma, isiyokuwa na jina wala cheo cha aliyeandika, huku habari ya Pambazuko ikitajwa kuwa ni “taarifa” – Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakanusha kuwepo kwa wizi na ufisadi kwenye mnada huo, huku ikishindwa kupinga kilichoandikwa na Pambazuko.

Msingi wa taarifa hiyo ya wizara ni kutaka kujisafisha kwa umma na kuonyesha mafanikio kidogo yaliyopatikana, wakati ukweli ni kwamba bila ufisadi katika mnada huo wa kimataifa, Hazina ya Tanzania, ingepokea kiasi kikubwa zaidi cha mapato, badala yake fedha nyingi zinaingia mifukoni mwa wachache kwa manufaa binafsi.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa waandishi wa Pambazuko, ambao walifika kwenye ofisi ya mkuu wa mnada huo Juni 12, mwaka huu, na eti kudanganya kwamba wametumwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ili kupata ushirikiano, hazina ukweli wowote, kwani wa-

tendaji wa gazeti hili wamejaa weledi, ufahamu na wanazingatia misingi mikuu ya taaluma ya uandishi wa habari.

Hivi waandishi wetu wanawezaje kudanganya wakati waliandika majina yao – kwenye kitabu cha wageni, wakitanabaisha wanakotoka na kusaini kitabu cha wageni saa 4:32 asubuhi? Kimsingi, taarifa ya kukanusha ya wizara ndiyo inapotosha na kudanganya umma.

Habari iliyochapishwa na Pambazuko, imebeba ukweli wa kinachotokea kwenye mnada huo, na ushahidi - hata ule usiokuwa wa kiuchunguzi zaidi, unaweza kuthibitisha haya kwa kufuatilia yanayotendeka kwenye mnada huo ambao watendaji wengi, wakishirikiana na baadhi ya vigo-gu wa wizara, wanalindana kwa ajili ya kuendelea kufisidi mapato yanayopaswa kuwa ya Watanzania wote, badala yake yanakwenda kwenye mifuko binafsi.

Pambazuko kwa kufuata misingi ileile ya taaluma ya habari, iliamua kutochapisha majina ya wezi wa fedha za umma katika Mnada wa Pugu ulioko Dar es Salaam kwa kuwa hawakutoa ushirikiano. Wengi walikuwa “wakikimbiakimbia” kukwepa waandishi wetu.

Na kwa kuwa Pambazuko siyo Polisi wala Takukuru, halikuona haja ya kuwataja, lakini

sasa tunaomba Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, apokee simu zetu na kushirikiana na Pambazuko ili iwe rahisi kumpa majina ya wezi wote kwenye mnada huo na washirika wao.

Sisi tumedhamiria kutimiza wajibu wetu kwa Tanzania, umma na hasa kiongozi wake, Rais Samia Suluhu Hassan, kupambana na wezi, mafisadi na makundi ya wala rushwa na madhila mengine yanayofifisha ustawi na neema kwa kila Mtanzania, na kamwe hatuwezi kuogopa “makanusho” na vitisho vingine vyovyote vilivyopo na vinavyokuja.



Balozi Battle atua kwa wakimbizi



*Balozi wa Marekani
nchini Tanzania,
Michael Battle
(mwenye koti lenye
maandishi ya USAID)
akitembelea kambi
ya wakimbizi ya
Nyarugusu, iliyoko
wilayani Kasulu,
Kigoma ambayo
inahifadhi wakimbizi
kutoka DRC na
Burundi. Balozi
alifurahishwa na
juhudi za mashirika
ya Umoja wa Mataifa
na washirika wake
kutekeleza mahitaji
ya kibinadamu
ya wakimizi wote
wanaoishi katika
mazingira magumu
nchini Tanzania.
(Picha na Ubalizi)*

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A - nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435;
Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*



Mwabukusi atikisa mdahalo TLS



Boniface Mwabukusi

Na Andrew MSECHU

MGOMBEA nafasi ya Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), Wakili Boniface Mwabukusi ‘ametikisa’ mdahalo kwa hoja, huku akionekana kung’ara miongoni mwa wagombea wengine watano.

Mwabukusi aliyerejeshwa kwenye kinyang’anyiro hicho na Mahakama Kuu - Masjala ya Dar es Salaam, baada ya awali kuenguliwa na Kamati ya Maadili ya TLS, alisema endapo atachaguliwa kuwa rais atafanya “mageuzi makubwa” ili chama hicho kibebe taswira na heshima kinachostahili.

Katika mdahalo huo ulioendeshwa na kituo cha luninga cha Star Tv ndani ya Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Saam, Jumamosi - Julai 27, mwaka huu, alisema endapo atachaguliwa kuongoza taasisi hiyo ya mawakili atahakikisha rasilimali za nchi zinalindwa kupitia Katiba na sheria zilizopo.

Mwongoza mdahalo huo, Edwin Odemba, aliibua suala la kuwepo Katiba mpya huku kila mgombea akitakiwa kulizungumzia kwa kuweka msimamo binafsi na pia wa taasisi anayotarajiwa kuongoza endapo atashinda.

Kwa upande wake, Mwabukusi alisema anaami-

ni TLS ni chombo kinachotakiwa kuelekeza nguvu zake kuwatetea na kuwapa msaada wa kisheria wananchi wote, hivyo akishinda atahakikisha anajenga kwa vitendo uwezo wa chama hicho kuwafikia wananchi wengi zaidi.

“Kuna vitu vya kushauri na vitu vya kushinikiza kwa nguvu za umma, ndiyo maana ya kifungu channe cha Katiba ya TLS...”

“Siyo kila kitu ni cha kubembebeza, vitu vya kushitaki tutakwenda mahakamani na kuna vitu tutawaambia Watanzania tusimame pamoja, sisi mawakili wenu tutakaa mbele tufuateni nyuma, hatutaki huo mkataba ufuteni, hamtaki hatutarudi nyumbani mpaka nchi iwe salama,” alisema Mwabukusi.

Kuhusu Katiba mpya, Wakili Mwabukusi alisema ili kushughulikia baadhi ya mikataba yenye utata ambayo nchi tayari imeingia, utatuzi wake utapatikana kupitia Katiba mpya pekee.

“Ni lazima tuanze na Katiba mpya ili kuwe na Katiba inayotambua umuhimu wa rasilimali za taifa na huo ndio urithi pekee tunaoweza kuutumia ili kurutubisha vizazi vinavyokuja.

“Hapo hatutakuwa na msalie mtume, hili ni jambo muhimu sana kwa sababu tumeshaumizwa kama nchi, hivyo msingi wa kwanza ni Katiba na moja ya maeneo tutakayotaka yafanyiwe kazi ni aina ya wabunge tunaoruhusu kwenda bungeni...”

1j“Kama kweli tunataka taifa letu libadilike, lazima twende kuangalia maeneo maalumu kwamba nani tunampa dhamana hii ya kutuwakilisha kwa sababu mikataba mingi ya kimataifa inapitia bungeni, lazima tuweke kinga ya kutosha, mwanasheria wa serikali atofautishwe awe ni mwanasheria wa nchi, siyo wa serikali,” alisema wakili huyo.

Mwanasheria huyo alisema Katiba ya sasa inamfanya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kujiona sehemu ya serikali, hivyo ofisi yake inatumika vibaya na kuendeshwa na nguvu za wanasasa wasiokuwa na utaalum wa sheria.

Aidha, kuhusu suala la Tanzania kushtakiwa kwenye mahakama za nje na kushindwa kesi mara kwa mara, Mwabukusi alisema hilo linatokana na

Inaendelea Uk. 6

Kampuni za simu zahemewa, zaomba msaada

Na Igo AI

BADO haijaeleweka endapo kampuni za simu za mikononi zimefurahi ama kuhuzunishwa kwa uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kupangua baraza lake la mawaziri wiki iliyopita.

Kampuni hizo ziko kimya. Hazijatanga za kupongeza uamuzi wa Rais Samia kugusa mabadiliko hadi wizara inayosimamia shughuli za kampuni hizo.

Hata hivyo, jambo moja ambalo jana limeibuliwa na Mtanzania mmoja, mkazi wa Barabara ya Mpakani A, Kijitonyama, Mzee Tai, kuhusu kampuni hizo ni kama vile zimefarijika mno kwa uamuzi wa Rais Samia.

Mzee Tai aliita waandishi wa habari na kuwaeleza amegundua kuwa kampuni hizo zimejaa furaha kwani alikutana na baadhi ya viongozi wao kwenye meza za kahawa na kusikia mazungumzo yao.

Kwamba alisikia wakielezana kwamba kampuni zao zimekuwa zikitingwa na kuhemewa na barua za michango kutoka kwa “wakubwa” wanaozisimamia, hasa wale wakubwa kabisa.

Kwamba wakubwa hao wa wizara - kila kucha, wamekuwa wakiomba michango ya majengo ya vyoo, barabara, majengo ya shule eti kusaidia majimbo yao ya uchaguzi.

“Mimi nimewasikia hawa ndugu zetu wa kampuni za simu wakisema, kwamba wamechoka kubeba mizigo ya michango kila mara, wanaombwa mno na wakubwa wa chama chetu na hata serikali, wao wanaombaomba tu, sasa wanasema wamechoka,” aliwasemea Mzee Tai.

Mzee Tai anadai kuwa matajiri hao wa kampuni za simu hawana shida sana kuchangia shughuli za maendeleo, lakini ilizidi; “kwamba hata harusi za wajomba na binamu wa wakubwa, nazo ilibidi kuchanga kwa kuwa walikuwa wakipelekewa bakuli na ni kama walikuwa

wakilazimishwa kuchanga.”


Mwandishi mmoja wa Pambazuko akauliza “sasa Mzee Tai, wewe unawasemea kama nani, wao hawana wasemaji wao?”

Mzee Tai: Hilo kawaulize wenyewe wanaogopa nini kusema kwamba wamehemewa na michango kutoka kwa wakubwa, ikiwamo ya mbio za mwenge, na sasa uchaguzi unakuja, watachanga sana kununua kura zenu.


Maswali yalipozidi, Mzee Tai alitanga za kumaliza mkutano wake na waandishi wa habari.

Na katika mkutano huo wa jana, Mzee Tai hakutoa hata maji ya kunywa, tofauti na mazoea ya mara kwa mara anapoita waandishi wa habari.

Tutumie tafsiri yako ushinde...



Huu ni mchoro wenye maana kubwa. Kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake, hivyo gazeti la Pambazuko linatafuta tafsiri fupi, inayoelezeka na kufanua vyema kuliko zote na itachapishwa na gazeti hili kwenye Ukurasa wa 30 toleo linalofuata. Mhusika atatumiwa zawadi – Tuma tafsiri yako kwa simu: 0744 768 263.



Mwabukusi atikisa mdahalo TLS

Inatoka Uk. 4

wanasheria kukosa uzalendo, kuogopa vyeo vyao kuliko wajibu wao kwa taifa na wanaogopa viongozi kuliko wanavyoogopa Katiba na sheria za nchi.

Wagombea wengine kila mmoja wakati akijibu swali kuhusu Katiba mpya, walieleza umuhimu wa kuwepo kwake ikiwa ndiyo njia sahihi ya kusaidia, kusimamia haki na utawala bora iwapo watachaguliwa.

Mmoja wa wagombea hao, Wakili Revocatus Kuuli alisema Katiba mpya na mchakato wake ulivyoanza, uwezekano wa kupata Katiba mpya ni sasa.

Kuuli alisema kuhusu mfumo wa kupata sheria na Katiba yenyewe, kifungu cha 4 cha Sheria ya Mawakili sura namba 307 kiko wazi kwamba wajibu wa mawakili ni kushauri serikali katika mwenendo mzima wa utungaji wa sheria.

Wakili Emmanuel Muga ambaye pia anawania nafasi hiyo ya urais, alisema suala la kuwa na Katiba mpya au kungoja, siyo la wakili wa TLS wala rais wa TLS kwa sababu siyo kazi yake.

“Kumekuwa na marais wanaokuja na jambo hilo na hakuna aliyeweza. Alikuwa nalo Tundu Lissu, lakini hakuliweza, akaja nalo Fatma Karume hakuliweza, akaja nalo Rugemeleza Nshala hakuliweza, tunaomba tumuangalie kwa makini huyu kwa kuangalia kuwa sisi kama mawakili na wanasheria tunafanya nini.

“Mimi siwezi kuzungumza hii hadithi ili kuwafurahisha watu, hili siyo suala la kupendezesha vijawe na hili suala halihitaji kuwa hadithi kwa ajili ya kuwafurahisha na kuwapendezesha watu wafurahie kwa kuwa ni jambo lisilowezekana,” alisema.

Mgombea mwingine, Wakili Sweetbert Nkuba alisema Katiba ya mwaka 1977 imefanyiwa marekebisho kidogo, waandishi wa Katiba ile walimtaazama Mwalimu Julius Nyerere wakati ule na kumpa nyenzo ya kufanyia kazi kwa matakwa yake, lakini Katiba ni kitu kinachoishi.

“Kwa hiyo kutokana na maendeleo yaliyofikiwa, Katiba ya mwaka 1977 ina mapungufu kwenye maeeneo mengi, ambayo inatakiwa itengeneze misingi ya kitaasisi ambazo zitaweza kujisimamia na kusiimamia serikali iweze kutekeleza majukumu yake.

“Chama cha wanasheria kama sehemu ya mahakama na kama mshauri mkuu wa serikali na bunge, moja ya agenda yetu kubwa itakuwa ni kuchochea mchakato wa Katiba mpya ambao ume-shaanza, kuhakikisha taifa linapata Katiba ambayo ni jumuishi itakayoakisi nyakati tulizo nazo,” alisema Wakili Nkuba.

Nkuba aliongeza kuwa wanasiasa na vyama ndiyo vinaokwamisha mchakato wa Katiba mpya kama ilivyotokea kwenye mchakato uliopata Katiba inayopendekezwa ambayo ilifikia wakati upinzani walitoka bungeni.

Aidha, Nkuba alisema pamoja na kwamba yeye ni mwanachama na kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), hawanii nafasi hiyo kama kada, bali anataka kufanya mabadiliko makubwa ndani ya TLS.

“Ninawania nafasi ya urais ndani ya TLS kama mwanataaluma, siyo nafasi kwenye chama cha siasa, kwa hiyo iwapo nitaipata, sitatumika kisiasa na nitahakikisha naitumia kufanya mabadiliko makubwa.

Ni wazi kuwa sisi sote hapa tuna itikadi za kisiasa tunazoziamini na tuna vyama vya siasa, hilo siyo kosa wala siyo dhambi, suala la msingi ni kufanya jambo sahihi linalotakiwa kuimarisha TLS yetu,” alisema. Wakili Ibrahim Bendera alisema endapo atachaguliwa atahakikisha TLS inaishauri vyema serikali kuhusu namna ya kuingia mikataba ambayo mwisho wa siku hupelekwa bungeni.

Wakili Paul Kaunda kwa upande wake alisema akiwa mtaalamu wa sheria kwa mujibu wa kifungu cha nne, ataendelea kushauri bunge kwenye masuala yote ya sheria na kwamba hakuna muswada unaokwenda bungeni bila kuwa na sehemu ya chama cha mawakili.

Alisema watakuwa makini kusaidia bunge na kama wakipuuza watatumia utaratibu wa kisheria kwenda mahakamani kushinikiza kusitishwa kwa mikataba itakayokuwa na sintofahamu.

Wagombea walioshiriki mdahalo huo ni pamoja na Ibrahim Bendera, Paul Kaunda, Sweetbert Nkuba, Emmanuel Muga, Revocatus Kuuli na Boniface Mwabukusi.

Pambazuko 'kupaishwa' zaidi na Rifaly

Na Mwandishi WETU

GAZETI pekee Afrika linaloandikwa kwa Kiswahili na kusambazwa kwa njia ya WhatsApp, Pambazuko kuanzia leo litakuwa likipatikana pia kupitia mfumo wa "App" ya Rifaly.

Hatua hii mpya ni njia nyingine kwa Pambazuko kuwafikia wasomaji wengi zaidi duniani, kwani Rifaly wamejenga mfumo wa kusambaza magazeti kwa urahisi na uhakika kwa watu wengi zaidi bila kujali mahali waliko duniani.

Gazeti la Pambazuko limefunga mkataba wa mwaka mmoja na Rifaly, kupitia kampuni yake mama, Smart Foundry ya Dar es Salaam, ambayo ni sehemu ya kampuni ya kimataifa ya Smart Africa Group (SAG).

Kufuatia mkataba huo, sasa Pambazuko linaweza kusomwa kupitia; www.rifaly.com, App ambayo pia inasambaza magazeti mengine ya Tanzania na nje ya nchi.

Mhariri Mkuu wa Pambazuko, Simon Mkina akizungumza baada ya kusainiwa kwa mkataba huo wiki iliyopita, alisema kuwa uongozi na watendaji wote wa gazeti hilo wamepokea kwa furaha uamuzi wa kufunga mkataba na kwamba sasa "gazeti la umma," litafikia wengi zaidi.

Mhariri Mkina alisema kuwa Pambazuko litaendelea kupatikana bure na hakutakuwa na mabadiliko ya maudhui, isipokuwa sasa nguvu itaongezwa katika kusambaza gazeti hilo linaloongoza kusomwa zaidi na wanaokifahamu au kujifunza Kiswahili duniani.

Mwanzilishi wa Biashara wa Smart Foundry, Loth Makuza ambaye alisaini mkataba huo kwa niaba ya kampuni yake, alisema kupatikana kwa Pambazuko katika kanzidata yao, ni hatua kubwa ambayo walikuwa wakiisubiri kwa hamu na muda mrefu.

"Tumepokea kwa furasa zaidi hatua hii ya kuan-

za kusambaza Pambazuko, kwani tumegundua kuwa umma wa Watanzania na wale wa mataifa mengine, wamelipokea na kulikubali gazeti kwa kuwa linaandika wanayokosa mahali pengine," alisema Loth.


Loth alisema kuwa Watanzania wana kiu ya kupata habari zaidi zilizofanyiwa kazi, ambazo kwa muda mrefu walizikosa, sasa wanazipata kupitia Pambazuko.



Mhariri Mkuu wa Pambazuko, Simon Mkina (aliyevaa shati jeupe), akibadilisha mkataba na mwakilishi kutoka Rifaly, Loth Makuza katika ofisi za gazeti hilo jijini Dar es Salaam wiki iliyopita. (Na mpiga picha wetu)



Habarika kidijitali! Soma gazeti la Pambazuko na magazeti mengine maarufu kwenye Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com





Wizara yakwepa kuzungumzia ubadhirifu Mnada wa Pugu



Prof. Daniel Mushi

Na Mwandishi WETU

ZAIDI ya wiki mbili sasa, maofisa wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wamekuwa wakikwepa kuzungumza na waandishi wa gazeti la Pambazuko kuhusu tuhuma za ubadhirifu mkubwa wa fedha katika Mnada wa Mifugo wa Kimataifa wa Pugu, Dar es Salaam.

Baadhi ya maofisa waandamizi wa wizara hiyo wanapopigiwa simu wanakataa kuzungumza, pindi wanapoelezwa kuwa aliyepiga ni mwandishi wa habari wa gazeti la Pambazuko.

Siku kumi zilizopita mwandishi wa Pambazuko alifanikiwa kumpata – kwa njia ya simu, naibu katibu mkuu wa wizara hiyo anayeshughulikia mifugo, Prof. Daniel Mushi, ambaye aliombwa kutoa ufafanuzi kuhusu tuhuma za ubadhirifu katika mnada wa Pugu, alimweleza mwandishi kwamba gazeti hili liachane na habari hiyo eti “inawachafua watu.”

Alipoelezwa kuwa nia ya Pambazuko siyo kumchafua mtu yeyote, bali kusaka ukweli kuhusu

tu tuhuma hizo, kiongozi huyo wa umma alisema kwa wakati huo asingeweza kutoa ufafanuzi wa kina kwa sababu alikuwa njiani kuelekea Dodoma.

Prof Mushi akakubaliana na mwandishi kuwa akifika Dodoma watapanga miadi ya kuzungumzia suala hilo kwa undani.

Pambazuko lilimweleza naibu katibu mkuu huyo kuwa lipo tayari kutuma mwandishi wake kwenda Dodoma iwapo atahitaji kukutana naye ana kwa ana huko.

Hata hivyo, tangu Jumatatu ya wiki iliyopita jitihada za Pambazuko kuwasiliana na kiongozi huyo kwa njia ya simu ya kiganjani zimegonga mwamba.

Mara kadhaa alipigiwa simu lakini iliita bila kupokelewa. Hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maandishi kwenye simu yake ya kiganjani, licha ya kuonesha kuwa ujumbe huo umepokelewa, lakini hakujibu chochote hadi tunakwenda mitamboni jana.

Katibu atembelea Pugu

Baada ya habari ya Pambazuko katika toleo lake la 79 kuibua tuhuma za ubadhirifu na kuto-tekelezwa kwa sehemu kubwa ya maagizo yaliyotolewa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, naibu katibu mkuu huyo, Prof. Mushi alitemebela mnada wa Pugu kwa kile kichoelezwa kuwa kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Waziri Ulega aliyoyatoa Desemba 2023.

Prof. Mushi alieleza baada ya ziara hiyo kuwa; “kwa asilimia zaidi ya 90 maagizo yaliyotolewa yametekelezwa kwani taa zimewekwa, choo kipya kimejengwa kwa kushirikiana na halmashauri na maduhuli ya serikali yameongezeka...”

“Kwa takwimu zilizopo kabla ya Desemba 2023, tulikuwa tunakusanya (shilingi) milioni 100 kwa mwezi, baada ya kuunda timu mpya na kufanya usimamizi mapato hayajawahi kushuka chini ya (shilingi) milioni 200...”

Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



‘Ngoma’ sasa iko kwa Trump vs Kamala Harris

KAMA ilivyoenezwa kwenye safu hii wiki chache zilizopita kwamba Rais Joe Biden wa Marekani, ambaye alitarajiwa kuwa mgombea urais kwa tike-ti ya chama chake cha Democrats, lakini alikuwa akikabiliwa na shinikizo kwamba ajiondoe, hatimaye amefanya hivyo.

Moja ya sababu zilizosababisha shinikizo hilo kwa Biden ni jinsi alivyoboronga kwenye mdahalo kati yake na mgombea wa chama cha Republican, Donald Trump.

Katika mdahalo huo, Biden alionekana kushau maneno sambamba na kuongea maneno yasiyoeleweka, na licha ya Trump kutumia muda mwingi kueleza mambo yasiyo ya kweli, alionekana kushinda kirahisi mdahalo huo.

Lakini, hata kabla ya mdahalo huo, kura za maoni zilikuwa zikionyesha kuwa Trump yupo mbele ya Biden.

Kana kwamba hiyo haikutosha, Biden aliendelea kukosea vitu mbalimbali katika matukio yaliyokuwa yakifuatiliwa na wengi.

Mfano mmoja ni kuwepo kwa ‘clip’ inayomonyesha akichanganya kutamka jina Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskyy, na kumuita Putin.

Baadaye ikaonyeshwa kuwa badala ya kumtaja makamu wake wa rais kuwa ni Kamala Harris, Biden alimtaja kuwa ni Trump.

Taratibu shinikizo lililoanzia kwa viongozi wachache tu wa chama hicho lilianza kukua na kusambaa, na kwa hakika uamuzi wake wa kujiondoa kwenye kinyang’anyiro hicho ulikuwa haiepukiki.

Kama ilivyotarajiwa, kujiondoa kwa Biden kumetoa fursa kwa makamu wake, Harris, kupeperusha bendera ya chama hicho kwenye uchaguzi mkuu wa nchi hiyo utakaofanyika mapema Novemba, mwaka huu.

Ujio wa Harris unaelekea kubadili mwelekezo wa uchaguzi huo. Awali, Trump mwenye miaka 78 alikuwa akimkebehi Biden mwenye miaka 81

kuwa ni mgombea mzee kuliko wote katika historia ya Marekani.

Hata hivyo, “kibao kimemgeukia” kwani yeye sasa ndio anashikilia rekodi hiyo aliyokuwa akiitumia kumdhihaki Biden, kwani Harris ndio kwanza ana miaka 59.

Wagombea hawa wawili wana fursa na changamoto, zinazotofautiana kulingana na maeneo kadhaa.

Kwa upande wa Harris, changamoto kubwa kwake ni ukweli kwamba hawezi kukwepa rekodi yoyote mbaya kuhusu utawala uliopo madarakani kwa sababu yeye ni sehemu ya utawala huo.

Na katika hilo, eneo moja linalotarajiwa kuwa changamoto kwake ni uhamiaji haramu.

Fursa kubwa kwa Harris ni wapigakura vijana. Ujio wake umeleta msisimko mkubwa kwa vijana mbalimbali, wakiwamo wenye asili ya Bara Hindi, Afrika na hata wazungu wengi wanaonekana “kumkubali.”

Kwa Trump, changamoto kwake ni pamoja na matatizo ya kisheria yanayomkabili.

Harris, ambaye kitaaluma ni mwendesha mashtaka, amekuwa akimuita Trump mhalifu na kumtaja kuwa Marekani haiwezi kuongozwa na mtu mwenye rekodi chafu ya uhalifu ambao uko kwenye rekodi rasmi.

Moja ya fursa kwa Trump ni “u-mungu mtu” wake miongoni mwa wafuasi ambao wanamkubali bila kujali lolote.

https://instagram.com/evarist_chahali



Kamala Harris



Donald Trump



Tafakuri ya Bagonza

Nchi haiwezi kupoa kama ugali!



Ugali

Na Dkt. Benson BAGONZA

MZEE mmoja ninayemheshimu, juzi kanipigia simu kunipa ugua pole. Katika kuongea nikamwuliza vipi huko Tanzania mnaendeleaje? Akanijibu, “Baba Askofu, nchi haipoi kama ugali”.

Akafafanua, “ugali ukipoa ni umepoa wote. Lakini nchi yaweza kupoa juu huku ndani kuna fukuto la moto”.

Nakubaliana naye ninapotafakari haya yafuatayo;

Kwamba rais amefungua nchi, lakini kuna wenye “funguo malaya”, wanaifunga tena. Mgeni anakutana na rushwa uwanja wa ndege mara anapoingia.

Huyu akiondoka atarudi tena? Mwekezaji wa ndani na wa nje anakumbana na masharti kuliko makaribisho. Wanaofunga wanaonekana kuwa na nguvu kuliko nguvu anayefungua.

Kwamba rais ameiunganisha nchi, lakini kuna wanaoigawa na kuitawanya. Zile 4R za rais, wao wanazigeuza na kuwa 4D - divide, dismiss, dillute na diverge. Tunagawanyika na kupoteana.

Kwamba rais ameahidi uchaguzi huru na wa haki; lakini kuna waliozoea kuiba kura wanasema hata yeye walimuibia za kumtoshia, na akileta ubishi wataiba za kwake arudi Kizimkazi! Mazoea yana taabu. Watu wanaiba na kusahau walikoficha.

Kwamba rais amesisitiza utawala wa sheria, lakini watu wanateka watoto wa watoto. Hali ilivyo, waweza kurudi nyumbani ukitokea kuteka, ukakuta mtoto wako ametekwa. Kibaya zaidi, wanaotuhumiwa kuteka, wanajipa kazi ya kuchunguza utekaji!

Kwamba rais amesisitiza tuanze ukurasa mpya wa upendo. Sasa tunapendana mpaka “tunapeana sumu” mitandaoni.

Ukitaka kujua unapendwa, zima simu juma zima, utawajua wanaokupenda na kukuchukia. Siku nikifa natamani Mungu aniachie kadirisha kadoogo ka kuona wapendwa wangu wanavyolia.

Kwamba rais amesisitiza kutanguliza maslahi ya taifa kuliko ya matumbo yetu yasiyoshiha. Kuna watu ni matajiri kuliko wizara zao, mashirika na vitengo vyao.

Kibaya, kuna watu ni matajiri kuliko rais! Mama zingatia; hakuna tajiri mtiifu kwa masikini. Kuna siku utatumbua, upate majinamizi kuwa umetumbuliwa.

Kwamba rais amesisitiza yeye ni wa awamu ya sita. Wakongwe na wajuzi wamekomalia, hii ni awamu ya tano.

Upinzani wa wapinzani ni cha mtoto. Mtumbwi wa kijani umetengenezwa kwa muhogo. Kuna panya wanakula mtumbwi tuzame wote. Sumu ya panya haitoshi. Tujadiliane.

Kwamba rais amesisitiza, mafanikio yawe ya chama. Machawa wamekazana ni ya mama. Tukiwaacha watadai mama ni wa kwao tu, sisi ni wa kambo!

Kama mama kafanya kila kitu, nyie kura mnataka za nini? Tutapiga moja kwa yeye afanyaye kila kitu. Machawa msisubiri awaumbue. Mafanikio yameletwa na kodi zetu na kura zetu zilizoibiwa na zilizobakizwa.

Mama asimalize utumbujaji, watasinzia. Kama huoni vizuri, niulize nitakuonyesha.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kilutheri la Kiinjili Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Ulevi wa madaraka, mbaya kuliko pombe

KAULI aliyoitoa hivi karibuni aliyekuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, huko Kashai, Bukoba, Kagera, imeibua mjadala mkubwa kuhusu tabia ya ulevi wa madaraka walionayo baadhi ya viongozi.

Msemo wa Kiswahili unaosema “heri kulewa pombe kuliko kulewa madaraka” unafafanua vizuri hisia hizi, ukiashiria kuwa ulevi wa madaraka unaweza kuwa na athari mbaya zaidi kwa jamii kuliko hata ulevi mwingine.

Ingawa hoja yangu haina uhusiano wa moja kwa moja na hatua ya Rais Samia Suluhu Hassan kumvua madaraka kiongozi huyo, lakini nitatumia msemo huu wa Kiswahili kama msingi wa hoja yangu.

Kulewa madaraka ni hali ya kiongozi kuwa na kiburi na kudharau wajibu wake kwa wananchi.

Ni hali ambayo kiongozi anatumia cheo alichonacho kwa manufaa binafsi au kwa namna isi-yostahili, na kusahau kwamba cheo ni dhamana inayotakiwa kutumika kwa maslahi ya umma.

Kauli ya Nape inaweza kuashiria kulewa madaraka, ambapo alijiona kuwa juu ya wananchi na viongozi wenzake.



Nape Nnauye

Alisema; ”matokeo ya kura siyo lazima yawe yale ya kwenye boksi la kura. Inategemea nani anayehesabu na kutangaza...”

“Na kuna mbinu nyingi, kuna halali, kuna nusu halali na kuna haramu. Na zote zinaweza kutumika, ilimuradi tu ukishamaliza, unamwambia Mwenyezi Mungu nisamehe pale nilipokosea.”

Kauli hii ya Nape ilikuwa na mkanganyiko na ukosefu wa nidhamu, siyo tu kwa Watanzania, lakini pia hata kwa Rais Samia ambaye ameoneka na kufanya jitihada za kurejesha utangamano wa kisiasa hapa nchini kwa kutumia falsafa ya ‘R NNE.’

Ni kauli mbaya pengine kuliko hata ile iliyowahi kutolewa na waziri mmoja kuwataka Watanzania wakaishi Burundi kama wanaona hapa nchini kodi zimekithiri!

Viongozi waliokunywa vyeo na kulewa madaraka aghalabu hupoteza uadilifu, heshima, na wanashindwa kuongoza kwa kufuata maadili ya uongozi bora.

Pombe inaweza kumuathiri mtu binafsi kwa muda mfupi, lakini kulewa madaraka kunaathiri jamii nzima na kwa kipindi kirefu zaidi.

Kiongozi aliyelewa madaraka anaweza kuleta uharibifu mkubwa na kudhoofisha mifumo ya kiutawala na kijamii.

Kwa kutumia msemo huu wa Kiswahili, tunaweza kuona kwamba kulewa madaraka ni tatizo kubwa katika uongozi.

Kauli ya Nape ilikuwa na dalili ya kulewa madaraka, na hatua ya Rais Samia Suluhu Hassan kumtumbua ni mfano mzuri wa jinsi viongozi wanavyopaswa kuwajibishwa.

Ni muhimu kwa viongozi kuwa na unyenyekevu, kuheshimu madaraka waliyokabidhiwa, na kuwatumikia wananchi kwa uadilifu na uwajibikaji, badala ya kuonesha dharau, majivuno na kibri!

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com

Ni aibu Afrika kusujudia Ulaya, Marekani – Profesa Maina

Na Peter NYANJE

VIONGOZI wa Afrika, wamelaumiwa kwa “kusujudia” na “kuwalamba miguu” wakuu wa nchi tajiri.

Mhadhiri wa sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Chriss Peter Maina amewashukia viongozi wa nchi za Afrika kwa vitendo vyao vya “kujikomba” kwa nchi tajiri.

Akizungumza mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Prof. Maina alisema ni aibu kwa viongozi wa Afrika, bara lenye utajiri mkubwa, kukimbizana kwenda kwenye nchi moja barani Ulaya au Marekani kwa matarajio ya kupata misaada na mikopo.

Alisema utaratibu wa nchi moja inayojiona tajiri kuwaita viongozi wote wa Afrika katika kile kilichopewa jina la mkutano baina ya nchi hiyo na Afrika, ni utaratibu wa kuziabisha nchi za Afrika.

“Nyie nchi 54 mnapokwenda wote mnakusanika kwenye nchi moja kusikiliza mtakachoambiwa, ina maana kuwa nchi hiyo ni muhimu kuliko bara lote la Afrika, hii ni aibu kubwa,” alisema Prof. Maina wakati akizungumza na Pambazuko pembeni ya mkutano uliojadili masuala ya ushirikiano wa Tanzania na Urusi.

Mkutano huo uliofanyika wiki iliyopita ni mwendelezo a mikutano ya aina hiyo inayoandaliwa na Klabu ya Valdai, ambayo ina utaratibu wa kuwakutanisha watalaamu na viongozi kutoka Afrika na Urusi kujadili mambo mbalimbali.

Urusi ni moja ya nchi zenye utaratibu wa kukutana na viongozi wa Afrika kujadili masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii na wakati mwingine ya kisiasa.

Wananchi wanapuuzwa

Prof. Maina alisema kitu kibaya zaidi ni kuwa



Prof. Chriss Peter Maina

viongozi wa Afrika wanapokwenda kwenye mikutano hiyo wanakuwa na mahitaji tofauti na yale yanayotakiwa na wananchi wao.

“Ukiwauliza wananchi wa kawaida hivi sasa kama twende mahali tukakope watakuambia hapa na. Watakuuliza kwa nini tukakope wakati sisi tuna rasilimali zinazotuwezesha kujitegemea?” Alisema.

Prof. Maina alisema tatizo hilo linatokana na wananchi kutokuwa na nguvu ya kuwawajibisha viongozi wao baada ya kuwachagua.

“Hapa kwetu kiongozi mkishamchagua tu, anaacha kuwatumikia na hamna la kumfanya mpaka uchaguzi mwingine,” alisema.

Profesa huyo alishangaa kwa nini viongozi wengi wa Afrika wanakwenda kukopa wakati hao wanaokopesha wanapata fedha kutokana na rasilimali zilizopo Afrika.

Biashara ndio mkombozi

Prof. Maina alisema mkombozi mkubwa wa Afrika, ukiacha mawazo ya viongozi, ni biashara.

Alisema ili kuepuka kunyonywa na nchi zinazotangaza kutaka kuisaidia Afrika, nchi za bara hilo zinaweza kufanya biashara ya usawa zenyewe na kunufaika kuliko kufanya biashara na nchi kubwa.

Prof. Maina alisema Afrika ina karibu kila kitu kinachohitajika ili kuendelea, kinachotakiwa ni kuhakikisha unakuwepo mfumo mzuri utakaoziwezesha nchi za Afrika kuuziana bidhaa na huduma wao kwa wao.

Viongozi wa Afrika wamekuwa wakilaumiwa kwa “kukumbatia hofu”, hivyo kushindwa kuthubutu kuanza biashara miongoni mwao.

Kona ya Dkt. Bisimba

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA

WIKI iliyopita mjadala mkubwa katika mitandao ya kijamii ulikuwa ni kuhusu kutenguliwa uteuzi wa aliyekuwa Waziri wa Habari, Teknolojia na Mawasiliano, Nape Nnauye ambaye alitukejeli na kutudhihaki sisi wapiga kura.

Awali, watu wengi walimtaka ajiuzulu au mamlaka ya uteuzi itengue uteuzi wake. Katikati ya mijadala hiyo tulikutana na mabadiliko ya baraza la mawaziri na viongozi wengine wa serikali.

Katika mabadiliko hayo, aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Slaa, aliamishiwa wizara hiyo aliyokuwa akiiongoza Nape.

Vile vile uteuzi wa January Makamba aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na na Ushirikiano nao ulitenguliwa.

Pamoja na utenguzi huo, lakini bado kuna maswali kwamba kweli Nape amewajibishwa? Sisi wananchi ambao ni wapiga kura tuliona ametufanyia kosa kubwa sana.

Iwapo ni uwajibishwaji, je, huyu January Makamba naye amefanya nini?

Ningetegemea endapo huu ulikuwa ni uwajibishwaji, huyu mhusika Nape awekwe wazi kuwa kutokana na yale aliyoyatamka, akiwa Kagera ambayo yalikuwa ni kinyume kabisa na msimamo wa chama chake, na pia ni kinyume cha sheria na taratibu za uchaguzi na pia ni kinyume kabisa na suala zima la demokrasia, ndiyo maana uteuzi wake umetenguliwa.

Na hii ilitakiwa ionekane kuwa ni fundisho kwa wale wote wanaopewa madaraka, kujua mambo ya kuyaongea kwa wananchi na iwapo hawawezi kuwa hivyo, hawastahili kuwa viongozi. Pia angetakiwa aombe radhi ya kweli siyo ile aliyoitoa ya 'kikejelikejeli'.

Kinyume na hapo tukiangalia tunaona jinsi mamlaka za nchi hii zinavyotuchukulia Watanania kuwa wanaweza kumuweka kando huyu waziri ili kupooza mjadala na kama tulivyoo-na watu wengi wamefurahia kuwa angalau ameachwa, ametenguliwa.

Iwapo nchi yetu inataka iendeleo na kukua kidemokrasia, na tukijua kuwa iwapo tuna demokrasia ya kweli hata maendeleo ya watu yataongezeka, basi inabidi tubadili njia tunazotumia katika kuiishi demokrasia.

Utenguzi wa Nape ni kiini macho

Msingi mkubwa wa demokrasia ni watu na heshima kwao. Tunavyofahamu demokrasia ni utawala wa watu uliowekwa na watu kwa ajili ya watu.

Mamlaka ya uteuzi na utenguzi nayo ipo chini ya watu kama Katiba yetu ibara ya nane inavyoelezea.

Ikiwa hivi ndivyo mamlaka hiyo ya juu yaani rais, anapaswa kusikiliza kutoka kwa watu ambao ndiyo chanzo cha mamlaka yake.

Kama kauli ya Nape haikuwa sahihi, basi mamlaka ichukue hatua sahihi za kumwajibisha na kurekebisha.

Vinginevyo itaonekana kuwa huyu alikuwa sahihi mbele ya macho yao ila alitumia hadhara isiyo sahihi, hivyo badala ya kuwajibishwa anapumzishwa kidogo na kwa vile watu huonekana kusahau, baadaye aweze kurejeshwa.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwana-harakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.



Nape Nnauye

 Habari

Wizara yakwepa kuzungumzia ubadhirifu...

Inatoka Uk. 8

“Mnada huu tuliweka malengo ya kukusanya (shilingi) bilioni 2.4 kwa mwaka, na hadi kufika Desemba 2023 zilikusanywa (shilingi) milioni 700. Baada ya maboresho na kubadilisha uongozi, zimekusanywa (shilingi) bilioni 1.3, hii ni mara mbili ya makusanyo ya awali...”

“Tunafurahi maelekezo tuliyoyatoa yamefanyiwa kazi, maboresho haya tutayafanya kwa minada yote hapa nchini na yatakuwa ni endelevu,” alisema Prof. Mushi wakati wa ziara hiyo.

Hata hivyo, alichoshindwa kubaini Prof. Mushi ni kuwa sehemu kubwa ya maagizo hayo hayajatekelezwa kikamilifu.

Mathalan, kuhusu kuweka taa ili mnada ufanya kazi mchana na usiku, taa alizoambiwa zimewekwa hazitoi mwanga wa kutosha nyakati za usiku kuweza kumulika vyema kwa kuwa alienda mchana alishindwa kulibaini hilo.

Aidha, licha ya choo kujengwa, lakini hakuambiwa kuwa kuna uhaba mkubwa wa maji mnadani hapo na kusababisha kero kwa watu wanaofika kuuza na kununua mifugo, na kufanya matumizi ya choo hicho kuwa kero.

Ingawa Prof. Mushi alieleza kuwa mnadani siyo mahali pa malisho, lakini mnada huo ulipaswa kuwa na sehemu ya kunyweshea mifugo jambo ambalo halifanyiki kutokana na uhaba wa maji.

Kuhusu suala la mapato, Pambazuko linazo taarifa kuwa ongezeko hilo la mapato analoeleza Prof. Mushi, dogo mno, kwani bado fedha nyingi zinaishia mifukoni mwa watu.

Takwimu zilizotolewa na serikali zinaonyesha kuwa makusanyo katika mnada huo yamevuka lengo kwa kuwa makusanyo yalifikia shilingi milioni 212 kwa mwezi kwa wastani. Lengo lilikuwa shilingi milioni 200.

Lakini takwimu kutoka mnadani hapo zinaonyesha kuwa kwa wastani ng’ombe 800 na mbuzi 500 huuzwa kwa siku.

Iwapo kiwango cha ushuru ni shilingi 7,500 kwa kila ng’ombe na shilingi 2,500 kwa kila mbuzi, basi makusanyo yanapasa kuwa shilingi milioni 292.5 kwa mwezi.

Kiwango hiki cha wastani kinazidi makusanyo ambayo serikali imeyaripoti.

“Tunafurahi maelekezo tuliyoyatoa yamefanyiwa kazi, maboresho haya tutayafanya kwa minada yote hapa nchini na yatakuwa ni endelevu,” alisema Prof. Mushi wakati wa ziara hiyo.

Pambazuko lina taarifa kuwa ikijumlishwa idadi ya mifugo inayochinjwa katika machinjio zote jijini Dar es Salaam, inazidi kwa kiasi kikubwa mifugo inayouzwa kwenye mnada wa Pugu.

Kanuni zilizopo zinaelekeza kuwa hakuna mifugo inayoruhusiwa kuingizwa katika machinjio yoyote Dar es Salaam bila kupitishwa katika mnada wa Pugu.

Ukiukwaji wa kanuni

Ufuatiliaji wa Pambazuko umebaini pia kuwa pamoja na madai hayo ya ubadhirifu, kuna ukiukwaji wa

miongozo na sheria zinazohusu minada ya wanyama nchini.

Moja kati ya mambo makubwa ya kikanuni yanayokiukwa ni kukosekana kwa mizani ya kupimia uzito wa mifugo inayouzwa mnadani hapo.

Pambazuko limebaini kuwa usimamizi wa wanyama hauko kama inavyotakiwa kwa mujibu wa miongozo ya minada ya mifugo nchini.

Moja ya vyanzo vyetu kiliainisha kuwa wanyama wote wanaochinjwa jijini Dar es Salaam wanasapaswa kufikishwa mnadani hapo kwanza na siyo kupelekwa moja kwa moja kwenye machinjio.

Machinjio ambazo zinapaswa kupata wanyama kutoka katika mnada huo ni Vingunguti, Ukon-ga, Tegeta, Kimara na Mbagala, huku Vingunguti ikiwa ndio machinjio kubwa inayopasa kupokea mifugo mingi kutoka katika mnada huo.

Moja ya chanzo chetu kilieleza kuwa mbuzi wanaotoka Mnada wa Pugu kila siku ni wastani wa 700 ingawa idadi ya wanaochinjwa Vingunguti pekee ni mara mbili ya idadi hiyo.

“Endapo naibu katibu mkuu ni mfuatiliaji mzuri wa mapato yatokanayo na mifugo, ajiulize kwa nini karibu asilimia 40 ya mifugo yote inayochinjwa kwenye machinjio za Dar es Salaam, haipitii Mnada wa Pugu kama sheria inavyotaka,” kilihoji chanzo hicho.

TRC yachafua Pambazuko, mhariri ang'aka



Mabehewa ya treni ya SGR

Na Mwandishi WETU

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC), limevimba na sasa linakaribia kupasuka kwa “kuguswa pabaya” na gazeti la Pambazuko kuhusu kutoa kandarasi ya kusafisha mabehewa ya treni ya kisasa ya mwendokasi (SGR).

Katika toleo lake namba 0081, lililochapishwa na kusambazwa Jumatatu iliyopita, Julai 22-28, 2024, gazeti la Pambazuko lilikuwa na habari iliyokuwa ikieleza kampuni ya Service Hub Tanzania, kupata kandarasi ya kusafisha mabehewa ya shirika hilo.

Pambazuko, bila kutia chumvi wala kushabikia, na kwa kufuata misingi yote ya uandishi wa habari za kiuchunguzi, liliandika kwamba Kampuni ya Service Hub Tanzania, iliyosajiliwa nchini, mwaka jana na kupata namba 168-765-258, imeanza kazi hiyo.

Hata hivyo, TRC haikufurahishwa na habari ile na kuanza kuchafua gazeti la Pambazuko kwenye mitandao ya kijamii.

Kuchafuliwa kwa Pambazuko kumemuibua mhariri wake mtendaji, Peter Nyanje, ambaye anahoji sababu za TRC kushindwa kutumia vyema taratibu za kukanusha habari kwa kuuliza gazeti husika, badala ya kudhalilisha chombo cha habari.

Nyanje anaitetea habari yake kuwa ina ukweli

wa asilimia 100 na kwamba TRC wameshindwa kujipambanua na kampuni zingine za mifukoni, badala yake imejishusha hadhi na kuitukanisha serikali kwa kudhalilisha Pambazuko.

Mhariri huyo mtendaji kufuatia kuchafuliwa kwa Pambazuko, amesema hana muda wa “kugombana na TRC,” lakini anahoji maswali kadhaa ambayo anaomba sasa yajibiwe na TRC.

1. Je, ni lini kampuni ya Service Hub Tanzania ilipewa kandarasi hiyo?
2. Je, kandarasi hiyo ilitangazwa wapi na lini?
3. Kampuni ngapi ziliomba kandarasi hiyo na ilikuwa na vigezo gani?
4. Je, Service Hub Tanzania ilishinda kwa vigezo vipi vilivyowekwa?
5. Je, Service Hub Tanzania imewahi kufanya kazi zipi na wapi za usafi?
6. Kazi hizo zilikuwa na ukubwa gani?
7. Je, kampuni ya Service Hub Tanzania wakati inapewa kandarasi ilikuwa imesajili ku-lipa VAT?
8. Kama haikuwa bado, ilipata vipi kandarasi hiyo?
9. Je, kwanini baada ya kuchapishwa kwa taarifa katika Pambazuko, TRC iliamuru kampuni ya Service Hub Tanzania kufuta tovuti yake mtandaoni?

10. Kulikuwa na kosa gani kwa Pambazuko kuandika kilichofungwa kwenye mkataba kati ya TRC na Service Hub Tanzania ili umma ambao ndiyo wenye mali, ujue?

11. Je, Pambazuko liliandika uongo? Na kama ni kweli, kwanini uongozi wa juu wa TRC umekuwa ukihaha kuficha mkataba huo?

12. Je, kuna uhusiano gani kati ya Service Hub Tanzania na Service Hub Kenya?

Nyanje ameomba kujibiwa kwa maswali hayo ili kazi zake zingine ziendelee kuhabarisha umma wa Tanzania kuhusu maendeleo ya TRC.

Katika toleo lake, Pambazuko liliandika kwamba zaidi ya shilingi milioni 4.8 zitakuwa zinalipwa kila siku na TRC kwa kampuni ya Service Hub Tanzania ikiwa ni gharama za kusafisha mabehewa yake 28.

Sumaye: CCM inaweza kuondolewa



Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye

Na Mwandishi WETU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), hata kama kinatamba kuwa kinafanya vizuri kutetea na kupigania maendeleo ya wananchi, kinaweza kuondolewa madarakani kwa “kuchokwa tu na watu.”

Akizungumza na Pambazuko katika mahojiano maalumu ofisini kwake Mwananyamala, Dar es Salaam, Sumaye alisema kuwa upo uwezekano mkubwa kwa CCM kuondolewa madarakani hata kama hakitafanya makosa.

“Kwa sababu katika mfumo wa vyama vingi, iko siku watu watakikataa chama hiki hata kama chama kinafanya vizuri kama malaika...”

“Watu kuna siku itafika watakikataa, watakapokikataa kama kule upande wa pili hakuna mwenye uwezo wa kubeba nchi, hapo sasa nchi inaweza kuingia kwenye vurugu,” alisema Sumaye.

Waziri mkuu huyo mstaafu, aliwataka Watan-zania kujenga vyama vya siasa vyenye nguvu ili

kuiwezesha nchi kuendelea kuwa imara hata pale ambapo chama tawala – CCM, kitaondolewa madarakani.

Sumaye alisisitiza kuwa kwa nchi iliyo katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, ni hatari sana kwa usalama wa nchi kuwa na chama kimoja kikubwa chenye nguvu huku vingine vikiwa havina nguvu wala uwezo wa kuongoza nchi.

Sumaye alisema msukumo wa kujenga vyama vya siasa vyenye nguvu ni moja ya sababu ziliyomfanya yeye kuondoka CCM na kujiunga na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

“Nimefanya kazi kubwa sana ndani Chadema. Nikagundua kwamba sifiki popote, badala yake ninakuwa sieleweki na wenzangu kule wakaanza tu kusema ooh huyu bwana ametumwa na CCM! Hivi mimi mtu mzima natumwaje na CCM?”

“Mimi nawafundisha siasa, nikawaambia mimi sijatumwa na CCM, nina nia njema, hiki chama tukibadilishe kiwe chama cha siasa, kisiwe cha uharakati. Kikiwa cha uharakati hatuwezi kuingia Ikulu,” alibainisha.

Hata hivyo, Sumaye alisema alishindwa kutekeleza lengo lake hilo kikamilifu baada ya baadhi ya watu ndani ya Chadema kuwa na fikra potofu kuhusu hatua yake ya kuhamia chama hicho.

Alisema wapo baadhi ya watu walidhani kuwa amehamia chama hicho kwa lengo la kutafuta cheo, hasa pale alipokuwa anashauri umuhimu wa kufanya mabadiliko ya uongozi ndani ya chama.

“Hapo ndiyo nilipogusa mboni ya jicho (anacheka) na shida ikaanzia hapo na ilikuwa kubwa,” alifafanua.

Rushwa

Akizungumzia rushwa kwenye vyama vya siasa, Sumaye anasema inasikitisha kuwa hivi sasa suala la rushwa kwenye uchaguzi limekuwa ni jambo la kawaida.

Akaongeza; “rushwa ni kubwa zaidi hivi sasa, tena kubwa sana - ni mbaya. Hata wewe leo ukitaka kugombea ubunge kitu cha kwanza watu watachokuuliza ni una hela?”

Alisema hali hiyo inasikitisha kwa sababu inasababisha ubaguzi kwenye uchaguzi, jambo ambalo siyo afya kwa demokrasia.

Polisi lawamani kunyanyasa Warundi

Na Mwandishi WETU, Kibondo

JESHI la Polisi Tanzania limelaumiwa kwa kunyanyasa raia wa Burundi ambao hufika maeneo ya wilaya za Kibondo na Kibondo, Mkoa wa Kigoma, kufanya kazi za muda mfupi na kurejea kwao.

Kiongozi (mstaafu) wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe ametoa lawama hizo kupitia ukurasa wake wa X.com (zamani Twitter) na kulisitaka jehi hilo kuacha tabia hiyo ya kunyanyasa raia wa Burundi wanaofika maeneo ya wilaya hizo kujitafutia riziki.

“Katika wilaya za Kakonko na Kibondo, mao-fisa wetu wa Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji, wanawasumbua raia wa Burundi wanaokuja kufanya kazi kwenye mashamba ya Watanzania...”

“Teleweke kuwa Burundi na Tanzania ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambapo wananchi wa nchi hizo wanaruhusiwa kutembea ndani ya nchi zinazoshirikiana kuunda umoja huo, bila kunyanyaswa,” amesema Zitto.

Taarifa zilizofika chumba cha habari cha Pambazuko zinaeleza kwamba baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi wilaya za Kakonko na Kibondo, wamekuwa wakinyanyasa raia wa Burundi wanaopokuwa wakihangaika kutafuta ajira za muda mfupi, hasa maeneo ya mashambani.

Kwamba raia hao huwalisi vijiji vya jirani zaidi na nchi yao, Burundi, kwa lengo la kupata kazi za kulima mashamba kwa ujira na baadaye kurejea kwao.

Zitto anasema EAC inaruhusu raia wa nchi wanachama, kupitia itifaki kadhaa za Soko la Pamoja (Common Market) kutembea watakapo.

Mwanasiasa huyo anasema wananchi wa wilaya hizo kwa kuwa na mashamba makubwa, wanahitaji nguvu kazi za ziada, hivyo inakuwa rahisi kuwapata wanaotoka Burundi, lakini baadhi yao wakinyanyaswa na polisi.

“Naomba protokali (itifaki) ya Soko la Pamoja iheshimiwe na watu hao wasinyanyaswe,” ameingiza Zitto.

Msomi atoa neno

Dkt. Mjega Kinyota, mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anasema hatua ya baadhi ya polisi kusumbua raia wa Burundi wanaofika kufanya vibarua, siyo haki.

Anasema kwamba baadhi ya askari hao hawana elimu ya kutosha kuhusu uhusiano ndani ya EAC.

“Ni vile tu wakoloni wametuwekea mipaka, lakini uhalisia wenyewe ni kuwa Warundi ni ndugu zetu; muhimu zaidi, tunaweza kushiriki pamoja shughuli za kiuchumi. Wenzetu wa Umoja wa Ulaya (EU) wametuzidi nini? Mbona wao wana-shirikiana zaidi? Tuna hofu zipi?”

Pambazuko limezungumza na Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime ambaye amesema askari wote wamefunzwa namna ya kuhudumia raia kutoka nje na kwamba wale wa maeneo ya mipakani, wanajua zaidi namna ya kutoa huduma, hivyo hana uhakika kama wanakwenda kinyume na taratibu za jeshi.



IGP, Camillus Wambura



Zitto Kabwe

Watoto wa kiume Tanzania hatarini

Na Mwandishi WETU

HALI sasa imebadilika. Watoto wa kiume wamebainika kuwa ndiyo wanaonyanyaswa zaidi kingono kuliko wasichana wadogo.

Wanaozungumzwa hapa ni watoto wa kiume wenye umri kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 12, na kwamba wanaohusishwa kufanya ukatili huo wa kingono ni ndugu na jamaa wa karibu na familia husika.

Uchunguzi wa Kituo cha Haki za Binadamu (LHRC) – Tanzania, uliochapishwa kwenye ripoti yake ya mwaka 2023, inaonyesha watoto wa kiume, kwa sasa wanaongoza kunyanyasika kingono.

LHRC imeeleza kuwa kati ya mwaka juzi; 2022 hadi 2023, jumla ya matukio 900 ya kulawitiwa yaliripotiwa katika taasisi na ofisi za Serikali, likiwamo Jeshi la Polisi.

Asilimia 80 ya matukio hayo ya watoto kulawitiwa – ikiwa ni sawa na watoto 720 yaliwahusu wavulana.

“Mkoani Dar es Salaam, iliripotiwa kuwa Julai, 2023 asilimia kubwa ya wavulana walipeleka kwenye mahakama ya watoto wakishtakiwa kwa makosa ya ulawiti jambo linalochangiwa zaidi na malezi mabaya, makundi mabaya na umaskini katika familia zao,” ilieleza LHRC.

Ripoti hiyo inaeleza kwamba wahusika wa kunyanyasa watoto ni pamoja na wazazi, ndugu wa karibu, watoto wenzao, walimu wa elimu ya msingi, walimu wa dini, majirani na watu wasiowafahamu.

LHRC inasema ukatili wa kingono hasa ubakaji na ulawiti ndio unaofanyika zaidi na wanaofanya matukio hayo wakiwa baba na baba wa kambo ambao huwa na nia ya kutekeleza vitendo hivyo kutokana na masharti wanayopewa na waganga wa kienyeji kwa ahadi ya kuwa matajiri au kupata nafasi za uongozi.

Kituo hicho cha haki za binadamu kinaeleza kwamba katika kipindi cha miaka saba, jumla ya

matukio ya ulawiti na ubakaji 57,335, kwa watoto yaliripotiwa katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2022.

Kwa hesabu hizo, ni kwamba matukio ya wastani wa 7,166 yalitokea kila mwaka na matukio 597 kila mwezi.

Mbali na matukio ya kingono kunyanyasa watoto, pia ukatili wa kimwili, ikiwa ni pamoja na kupigwa, kuchomwa sehemu za miili yao, kuteswa, kudhalilishwa na kutukanwa nayo yamebainika kuongezeka.

Ripoti ya LHRC inaonyesha kuwa watoto ndio wanaoendelea kuwa waathirika wakubwa wa matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu ambapo asilimia 45 ya matukio hayo yanawahusu wao, ikifuatiwa na wanawake (asilimia 30), wazee (12), wanaume (10), na watu wenye ulemavu (3).

Matukio ya ukeketaji

Ripoti hiyo ya LHRC inaeleza kuwa takwimu zinaonyesha kiwango cha matukio ya ukeketaji kimeendelea kupungua kutoka asilimia 18 ya mwaka 1996, hadi asilimia 8 ya 2022.

Idadi hiyo ni sawa na kueleza kuwa matukio ya ukeketaji yamepungua kwa asilimia 10, huku matukio hayo yakitajwa kufanyika zaidi katika mikoa ya Manyara (asilimia 43), Arusha (43), Mara (28), Singida (20), Tanga (19), Dodoma (18), na Iringa (12).



Anna Henga

Rukwa walalamika NFRA kuwakopa mahindi



Na Mwandishi WETU,

WAKULIMA wa mahindi kutoka Mkoa wa Rukwa wamelalamika kutolipwa fedha zao za mazao waliyoyauza kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA).

Wakizungumza na Pambazuko baadhi ya wakulima wameeleza kuwa hadi jana, ni zaidi ya wiki mbili tangu wauze mahindi ya, lakini hadi sasa hawajalipwa.

Maofisa wa ngazi za juu wa NFRA walikiri kuchelewa kwa malipo hayo wakisema kumesababishwa na kuchelewa kwa taratibu kadhaa za kifedha.

Akizungumza na gazeti hili kwa niaba ya wenzake, mmoja wa wakulima hao ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, alisema tangu wauze mahindi yao ni wamekuwa wakipigwa danadana bila kulipwa fedha zao.

“Ni zaidi ya wiki mbili sasa, hatujui tutalipwa lini. Tulipowapigia simu viongozi (wa NFRA) wa kanda walisema bado hawajapewa fedha...”

“Rais Samia alipokuja huku Rukwa alituhamasisha kwamba tuuze mahindi yetu NFRA na tumefanya hivyo. Lakini tunashangaa kwa nini tunapigwa danadana malipo yetu,” alihoji mkulima huyo.

Alisema kutokana na malipo yao kuchelewa, baadhi yao ambao hawajauza mahindi yao, wameanza kuyavusha mipakani na kuuza nchini Zambia kwa shilingi 40,000 kwa gunia.

“Ingawa malipo ni kidogo, lakini wale wanaouza mahindi yao Zambia wanalipwa hapohapo, lakini sisi tuliouza NFRA, ingawa tunapaswa kulipwa shilingi 70,000 kwa gunia, lakini hatujapata hela hiyo hadi leo...”

“Tunashangaa Rais Samia alipokuja hakutuambia kama tungeuza kwa mkopo mahindi yetu,” alilalamika.

Mkulima aliyeuza mahindi yake Zambia ambaye

naye hakutaka kutajwa gazetini, alisema alilazimika kuuza mahindi yake nchini humo baada ya kuona wale waliouza NFRA wanazungushwa kupata fedha zao.

“Nipeleke NFRA anilipe nani? Mwaka 1997 nilikutana na changamoto kama hii na hadi leo sijalipwa fedha zangu maana wakati ule kuna vyama viliibuka, tukapeleka mahindi huko, lakini hatukulipwa,” alisema.

Alipoulizwa endapo amefuata taratibu za kuuza mahindi Zambia alisema wao wanaishi mpakani hivyo wanauziana kama ndugu.

Akizungumza na Pambazuko, Meneja wa NFRA Mkoa wa Rukwa, Marwa Range, alikiri wakulima hao kutolipwa hadi mwishoni mwa wiki iliyopita.

Alisema hali hiyo imetokana na utaratibu wa malipo uliowekwa, ambapo mtu anayeua mahindi anapaswa kulipwa baada ya siku 14.

Alisema kuna baadhi ya wakuliwa walianza kulipwa Alhamisi iliyopita.

“Kuna malipo yameanza kufanyika jana (Alhamisi) na malipo ya wakulima yatakuwa yanaingia kwa awamu,” alisema Marwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NFRA wa Kanda, Dkt. Andrew Komba, naye aliliambia Pambazuko kuwa tayari wakulima hao wameshaanza kuingiziwa malipo yao.

“Kwanza utaratibu ni siku 14 kwa sababu lazima mahindi yakaguliwe, yapelekwe maabara na yakikidhi vigezo, ndiyo tunaanza kuwalipa wahusika. Sasa wao tangu wameleta mahindi bado haijatimia siku 14.

Rais Samia Suluhu Hassan Julai 16, 2024 wakati akizindua maghala ya kisasa ya NFRA katika eneo la Kanondo mkoani Rukwa aliagiza wakulima kulipwa shilingi 70,000 kwa gunia la mahidi watakalouza kwa wakala huyo.

Vilevile Rais Samia aliwataka wakulima kutosafirisha mahindi nje ya nchi bila vibali vya Wizara ya Kilimo na taratibu zingine ili kutoathiri uchumi wa soko la kibiashara.

Hata hivyo, hatua ya Rais Samia kuongeza bei wakati zwa ziara kumezua maswali kwani baadhi ya wakulima wanahoji kwa nini bei ya mahindi imeongezeka ‘ghafila’ wakati wa ziara ya Rais Samia.

Awali, kabla ya ziara hiyo serikali ilipanga kununua mahindi hayo kwa shilingi 500 kwa kilo.

Ana kwa Ana



Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olegurumwa, akizungumza na Mhariri Mkuu wa Pambazuko, Simon Mkina (wa kwanza kushoto) na waandishi wa habari wa gazeti hili, Elizabeth Hombo na Arodia Peter (kulia) wakati wa mahojiano maalum ofisini kwake Dar es Salaam. (Picha na Fidelis FELIX)

Olengurumwa: Sitamsahau Magufuli

ONESMO Olengurumwa ni miongoni mwa wanaharakati wa haki za binadamu wanaoheshimika kimataifa, ambao katika kutekeleza majukumu ya kazi, amekumbana na madhila mengi.

Wiki iliyopita Olengurumwa ambaye ni Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) alihojiwa na timu ya gazeti la Pambazuko, ambapo pamoja na mambo mengine amesimulia magumu aliyoyapitia wakati wa utawala wa Rais John Magufuli.

Pambazuko: Kuna changamoto gani ambazo THRDC inapitia katika kazi ya kutetea watetezi wa haki za binadamu nchini?

Olengurumwa: Changamoto zipo nyingi na ndiyo maana sisi tukawa tuko kwa ajili ya kuhakikisha mazingira ya utetezi wa haki za binadamu yanakuwa mazuri kuanzia kwenye sheria, mtazamo na kwenye utekelezaji wa kawaida wa kazi zetu.

Kazi zetu tunazifanyeje? Kwanza tunafanya ushawishi wa mabadiliko ya sera na vitu kama hivyo na pia tunafanya majadiliano na viongozi wa

serikali na wadau mbalimbali.

Mtandao tumeweza kukutana na viongozi wote wa nchi hii tangu tumekuwepo kwa miaka 13. Kwa mfano shughuli zetu zote zimeweza kufikiwa na mawaziri wote, mawaziri wakuu, hadi marais na Rais Samia (Suluhu Hassan) alikuwa ni mgeni rasmi wakati tunaadhimisha miaka kumi ya Mtandao wetu, Rais (Hussein) Mwinyi (Rais wa Zanzibar) naye alikuwa mgeni wetu rasmi wakati tunafungua ofisi zetu Zanzibar.


Lengo ni kuhakikisha kwamba tunashawishi sera, mifumo na mitazamo ibadilike kwa sababu tuna mitazamo tofauti na mingine mibaya kuhusu masuala ya haki za binadamu.

Kuna watu hawavipendi vyombo vya habari kwa sababu ya mitazamo, kuna watu hawatupendi sisi watetezi kwa sababu ya mitazamo, kwa hiyo tunajaribu kubadilisha kwamba sisi ni wadau tunaweza kufanya kazi pamoja.

Inaendelea Uk. 21



Habarika kidijitali! Soma gazeti la **Pambazuko** na magazeti mengine maarufu kwenye **Rifaly!**



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com





Olengurumwa: Sitamsahau Magufuli

Inatoka Uk. 20

Tunashukuru kwamba Rais Samia ametuelewa vizuri zaidi na ameweza kutembelea makundi yetu yote asasi za kiraia.

Ametuelewa vizuri kwamba sisi hatupaswi kuonekana tunashindanishwa au tunapambanishwa, na badala yake tuonekane ni wadau.

La pili ni kujengea uwezo watetezi kwa makundi yote niliyoyataja. Tumewajengea uwezo wadau wengi kuhusu masuala ya utetezi wa haki za binadamu ikihusisha namna ya ufuatiliaji na vitu kama hivyo na tunapozungumza hapa kwa miaka yetu 13, tumeweza kuwafikia zaidi ya watetezi wa haki za binadamu 6,000 kwa makundi yao yote kwa njia zetu zote.

Kikubwa sasa inapotokea mazingira kuwa magumu, kwa mfano, tumekuwa tukitoa matamko tukilaani ukiukwaji wa haki mbalimbali za binadamu, tumejaribu kufanya maandamano, haya yote ni katika kuhakikisha tu kwamba utetezi wa haki za binadamu unafikia katika hatua nzuri.

Pambazuko: Lakini pia mmekuwa mkienda mahakani kuhusiana na masuala haya ya haki za binadamu. Vipi huko kuna kesi ngapi?

Olengurumwa: Njia ya kwenda mahakamani ni njia mojawapo kama mliyoniuliza na kila mwaka sisi tunakuwa na kesi zaidi ya 10 ambazo tunazifungua sisi au tunawashauri na kuwasaidia mawakili wengine au Watanzania wengine kufungua kesi za mkakati.

Katika hilo tumeweza kutengeneza jopo la wanasheria zaidi ya 100 nchi nzima ambao wameonyesha interest (shauku) ya kusimamia hizi kesi, ndiyo maana unaona kesi zinaongezeka kwa sababu huwezi kuwa na kesi za mkakati kama huna mawakili ambao wanazielewa na wamejengea uwezo na hawana hofu kwa sababu wakati mwingine zinaonekana kama unapambana na serikali.

Hata mimi juzi nilikuwa na kesi pale Mahakama ya Rufaa. Ile kesi ya kuomba kwamba mashauri yasiende kwenye mahakama ambazo hazina mamalaka kwa mtu mwingine asiye mwelewa anaweza kufikiri unapambana na Serikali.

Lakini kwa mtu ambaye si mwelewa hawezi

kuelewa, ndiyo njia za kistaarabu ambazo tunapaswa kuzitumia isifikie hatua mfano Kenya zile njia walizotumia ndiyo wazione kuwa ni hatari.

Lakini unaenda mahakamani mnakaa mnaonea vizuri mnajadiliana mnapingana kwa hoja, baadaye jaji anasema wewe ndiyo umeshinda kwa hoja nadhani ni njia ambazo tunapaswa wote tuzi-one kwamba ni za msingi.

Kwa hiyo tunapozungumza kwa miaka yetu takriban 13 jumla inakuwa kesi 150 ambazo tumeshazifungua kwa njia mbalimbali kama kesi za kimkakati.

Sasa kuna zile zinazofunguliwa dhidi ya waandishi wa habari ambapo inatumika hizi sheria za mitandaoni.

Kuna kipindi tulikuwa tunasaidia siyo kesi chini ya 30 kwa mwaka ambazo watetezi wa haki za binadamu wamefunguliwa, wakiwemo waandishi wa habari.

Kipindi cha marehemu Magufuli (Rais, John) zilikuwa zinakwenda kesi nyingi zinazohusu hizi sheria za mitandao, zilikuwa zinakwenda hadi za money laundering (utakatishaji fedha).


Zilikuwa zinakwenda kwenye zile sheria za uhujumu uchumi kwa hiyo ziliongeza sana kesi.

Lakini sasa naona kama tumebaki na hizi za kawaida, za uchumi kidogo zimepungua maana yake zilikuwa kidogo zinatumiwa kwa kubambika

Inaendelea Uk. 22



Onesmo Olengurumwa



Ana kwa Ana

Olengurumwa: Sitamsahau Magufuli



Inatoka Uk. 22

watu.

Pambazuko: Tangu mlipoanza kazi hii ya utetezi wa haki za binadamu ni kipindi gani kilikuwa kigumu zaidi?

Olengurumwa: Tuseme tu ukweli kipindi kigumu kilikuwa cha awamu ya tano. kilikuwa kipindi ambacho kufanya kazi ya utetezi wa haki za binadamu ilikuwa ni kujiweka kwenye kitanzi.

Ilikuwa ni kujihatarisha wewe na familia yako na jamaa zako wote.

Ulikuwa ni uongozi ambao haukuthamini, haukuelewa, haukutambua chochote kuhusiana na masuala ya haki za binadamu.

Ni uongozi ambao haukutaka kukosolewa, haukutaka sauti mbadala kwenye jamii, ni uongozi ambao haukutaka kuona kiongozi wa nchi anakosolewa au viongozi wanakosolewa.

Katika mazingira kama hayo, lazima sisi watezi tuwe ni waathirika wakubwa kwa sababu ndiyo watu ambao tunakosoa.

Ule ni uongozi ambao nafasi ya raia ilikuwa imekufa kabisa na ndiyo makundi yote ya kiraia yaliuawa kwa namna moja au nyingine.

Vyama vya siasa viliauwa, sisi watezi wa haki za binadamu tuliua, maana yake ni kwamba tulishindwa kufanya kazi.

Waandishi wa habari waliuawa, viongozi wa dini nao kama vile waliuawa kwa hiyo mazingira yale yote yaliyofanya watu washindwe kufanya shughuli zao zilizotakiwa kufanyika kwa mujibu wa katiba na kwa mujibu wa sheria za nchi na katiba.

Ukiwanyima watu wasifanye shughuli zao, ku-

wanyima wasiseme, maana yake wale watu ni wafu, kwa hiyo kwa wakati ule tulikuwa wafu. Hatukuweza kusema.

Pambazuko: Hali hiyo iliathiri vipi shughuli za THRDC?

Olengurumwa: Nadhani mnafahamu tulikuwa kwenye hali mbaya, ni katika kipindi hicho baadhi ya watendaji wa kutetea haki za binadamu waliamua kutoka kwenye mchezo mapema.

Hata hivyo, sisi baada ya kuona hali ni ngumu, tukaendelea kukomaa na kusemasema hadi dakika tunakaribia uchaguzi, walitueletea barua nyingi za kutuzuia kufanya kazi.

Mikutano yetu ikaingiliwa dakika za mwisho wakaona wamalizie kwa kufunga akaunti zetu. Kama mlisikia walisema sisi tumefanya ugaidi.

Tukakaa miezi nane bila kuwa na fedha za kufanya kazi, lakini tukaendelea kuzungumza, kwa maana utetezi siyo fedha tu, tukaendelea kuzungumza kwa njia zingine huku tukiendelea kumwomba Mungu kwamba turudi kwenye kazi zetu.

Tunashukuru kweli, miezi nane ya kutokuwa kwenye kazi zetu, baadaye Rais Samia alikuja akatufungulia akaunti zetu pamoja na za wengine.

Lakini wakati mwingine changamoto zinapotukumba kama binadamu, hatupaswi kuziona kama ni sehemu ya kufa, bali tuzichukulie ni chachu ya kusonga mbele zaidi.

Sisi tulizichukulia hizo changamoto kuwa zimekuja kutuimarisha, zimekuja kutupa akili na nguvu na baadaye tukarudi kwenye kazi vizuri na tunaendelea na kazi zetu.

Tunaendelea kukosoa kiongozi yeyote aliye-po madarakani, asipofanya vizuri tutakosoa na atakayefanya vizuri kumtambua.

Tulimtambua Rais Samia kwa ile miaka yake miwili mwanzoni. Tulitambua kabisa kuwa alifanya vizuri kwenye zile jitihada zake kuhakikisha tunairudisha nchi kwenye mazingira yanayoheshimu haki za binadamu.

Wapinzani nao walianza kufanya kazi, kila mtu alijihisi kwamba nchi ni ya kwake, Rais Samia aliondoa zile hofu na akaja na zile R4, kwa hiyo

Inaendelea Uk. 23

Je wajua



Kuna maeneo sita duniani ambako jua halizami kwa zaidi ya siku 70, maeneo hayo ni Norway; Nunavut, Canada; Iceland; Barrow, Alaska Finland pamoja na Uswidi.



Nyegere ni moja kati ya wanyama wenye wivu sana hapa duniani, unaambiwa hata jani tu likimgusa jike litararuliwa. Chakula chake kikubwa ni asali, yeye hupanda juu ya mzinga wa asali na kupakua asali na masega yake na kula.

Olengurumwa: Sitamsahau magfuli

Inatoka Uk. 22

tukaona sasa ni sehemu ambayo tunaweza tukafanya kazi, ingawa bado changamoto zipo nyingi za kisheria.

Anachofikiria Rais Samia na misingi anayoweka, inaweza isieleweke, pengine bado kuna baadhi ya watu kule chini hawaioni kwamba ni misingi ya kwenda nayo kwa pamoja, hivyo unaweza kuna mkwamo kidogo wa maeneo machache.

Pambazuko: Je akaunti ya taasisi ilipofunguliwa mlikuta kiasi kile kile ambacho kilikuwepo tangu mwanzo?

Olengurumwa: Tunashukuru Mungu kwamba akaunti zetu tulizikuta ziko salama, ingawa jitihada zilifanyika nyingi sana za kutaka kuzipunguza hizo fedha kwa njia zile wanazojua wao.

Pambazuko: Nini mtazamo wako kuhusu maridhiano baada ya Rais Samia kuingia madarakani?

Olengurumwa: Tulimshauri Rais Samia kwamba kuwe na kamati ya haki na maridhiano ambayo itasahihisha na kufuta - angalau kidogo, machugu na madhara ya kuumizwa yaliyodfanywa kipindi cha Maguruli.

Kwamba yale yote yaliyofanyika, kwa mfano sisi hatukutendewa haki, tuliumizwa na bado tuna machungu lakini tumesamehe.

Wapo wengine ambao sasa hivi familia zao ni maskini, mfano wale waliokuwa wanafanyabiashara wa kubadilisha fedha za kigeni huko Arusha na Moshi, waliporwa hela zao zote kwa hiyo

bado kuna watu wana machungu.

Angalau sasa watu wajulikane waliofanya hayo. Bado wako hai ambao walishiriki haya tuhakikishe kwamba angalau wanaeleweka. Waombe radhi Watanzania kwamba walichokifanya hakikuwa sahihi.

Pambazuko: Bado mna mapendekezo hayo ya maridhiano kwamba waliohusika waombe radhi?


Olengurumwa: Kabisa. Huo ndiyo uongozi. Kule Afrika Kusini waliporudi kina Desmond Tutu (mwanaharakati aliyekuwa mstari wa mbele kupinga ubaguzi nchini Afrika Kusini) na kina Nelson Mandela (aliyekuwa rais), waliamua kuunda ile tume ya maridhiano na wale waliofanyamakosa walikiri, waliona walifanya makosa na kuomba msamaha.

Leo tunaona Afrika Kusini wanaishi kama wanavyoishi, vinginevyo ile nchi isingekalika kwa yale waliyokuwa wamefanyia wananchi wa Afrika Kusini wasingeweza kukubali kukaa na wale watu (makaburu)tena.

Lakini kutokana na utaratibu huo uliowekwa, hata Rwanda leo wananchi wake wanaishi kwa kuelewana na kusahau yaliyopita. Hili linapaswa kufanyika hata Tanzania pia.

Katika nchi ambazo zilitumbukia kwenye machafuko, hizo kamati zilisaidia sana, kwamba kila mtu analalamika, aliyefanya makosa anakuja, anaomba radhi na wanasameheana na kusonga mbele.

Inaendelea Uk. 25



Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL



Watanzania tuungane kukemea watoto kutekwa

HABARI kubwa na ambazo zinakera masikioni mwa watu kwa sasa, ni utekaji wa watoto wadogo.

Watoto wetu wanatekwa kila mahali, wanatekwa wakiwa njiani kuelekea ama kutoka shuleni, wanatekwa wakiwa mitaani katika viwanja vyao vya michezo na wengine wanatekwa wakiwa barabarani pindi wanapokuwa katika matembezi yao ya kawaida au wakiwa wame-tumwa kwenda dukani.

Mbeya wanalalamikia tabia hiyo, Dar es Salaam wanakemea uharifu huo, Arusha, Tanga Mwanza na kwingineko nchini, wazazi, walezi na watoto wenyewe, wamejaa hofu.

Vyombo vya dola vinakemea unyama huo, viongozi wa serikali wanaonya kuhusu suala hilo na kila Mtanzania anataka tabia hiyo ikomeshwe na wanaokutwa wakijihusisha na uharifu huo, wachukuliwe hatua kali za kisheria ili liwe fundisho kwa wengine wanaojihusisha na ukatili huo.

Yaani ukiangalia katika mitandao ya kijamii, ukisikiliza redio na ukiangalia televisheni na wakati mwingine ukisoma magazeti, moja ya habari zinazoshika kasi ni masuala ya utekaji wa watoto.

Ni habari mbaya sana hizo kwa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kwa sababu kila mmoja anathamini na kuheshimu haki za watoto ambao ni sawa na binadamu wengine.

Lakini ni habari mbaya pia kwa nchi kati-tika uso wa kimataifa, taswira ya nchi kuhusu kulinda haki za watoto inaharibika.

Kwa maana hiyo, ni wajibu wa kila mmoja wetu kuwa mlinzi wa kila mtoto huku kila mtu akitakiwa kuchukua hatua kadiri anavyoweza,

ili kuhakikisha utekaji huo unakoma kwa nam-na yoyote ile.

Viongozi wa makanisa ya Kikristo kwa upande wao, kila wanapohubiri neno la Mungu, wakumbuke kuwakumbusha waumini wao umuhimu wa kuwapa ulinzi watoto wao, iwe ni shuleni, mitaani na kwingineko wanakoweza kukutana na waharifu hao.

Waumini na jumuia nzima ielezwe kwamba utekaji wa watoto unakiuka haki za binadamu na pia Mwenyezi Mungu hafurahishwi na tabia hiyo kwa kuwa inapigwa vita kisheria na nchi zote duniani.

Kwamba ili watoto wawe salama, wanataki-wa kuwapa elimu ya kuwakwepa watu wasiowa-fahamu na pia wakumbushe watoto faida ya ku-rudi nyumbani kila wanapokuwa hawana kazi za kufanya shuleni na mitaani ambako ndiko watekaji wanakowakamatia.

Viongozi wa Kiislamu nao kila wanapohu-biri neno la Mungu, wahamasishe wananchi kujua faida na umuhimu wa kuimarisha ulinzi kwa wote kila wanapokuwa na pia wakumbushe waumini wao, kwamba ili utekaji wa watoto ukomeshwe nchini, kila mtu anatakiwa kuwa mlinzi wa kila mtoto.

Naamini kama hayo na mengine yatafan-yika kwa kuhusisha mamlaka zote wakiwamo walimu shuleni, watoto wetu watabaki salama na kuishi kwa amani na furaha kama walivyo-zoea.





Olengurumwa: Sitamsahau Magufuli

Inatoka Uk. 23

Kinachofanyika sasa baada ya msamaha, ni kuweka mikakati tusirudi tena kwenye hali tuliyokuwanayo awali.

Pia baada ya makubaliano hayo ya msamaha, sasa taifa linajipanga na kuapa kuwa sheria lazima zifuata, na kama zipo zenye kero au mbaya, zinarekebishwa.

Inawezekana kabisa kwamba watu walifanya uharamia mkubwa kwa kuwa sheria ziliwaruhusu, pia kuna watu walikuwa kama juu ya sheria.

Pambazuko: Unadhani Rais Samia anaweza kuridhia Katiba mpya?

Olengurumwa: Uwezekano upo katika mazingira makubwa yafuatayo; kwanza rais mwenyewe bado, kwa mujibu wa katiba tuliyonayo na mfumo wetu wa uongozi, ana mamlaka ya jambo lolote kubwa katika taifa letu.

Anaweza kuamka na kusema Katiba mpya ipatikane haraka, na jambo hilo likafanyika bila rabsha.

Pamoja na kwamba katiba tuliidai kwa miaka mingi, lakini ni hadi Jakaya Kikwete alipokuwa madarakani alipoamua mwaka 2014 kuanza mchakato wa katiba, kwa hiyo rais ana nafasi kubwa.

Lakini la pili; sisi kama Watanzania, tukiamua kuwa na Katiba mpya hata kesho inapatikana yaani wananchi tukiamua si mmeona Kenya?

Lakini uwezekano mwingine ni wa chama tawala kikiamua kuwatendea haki Watanzania, waibebe hii ajenda ya Katiba mpya ili waimalizie ilipoishia.

Pambazuko: Mbali na taasisi wewe binafsi uli-umizwa kiasi gani?

Olengurumwa: Mimi binafsi iliniuma sana pale ambapo umewatumikia Watanzania kwa nia nzuri, bila changamoto yoyote, anaposimama kiongozi mkubwa wa nchi anasema unafanya ugaidi na tunaunga mkono magaidi.

Binafsi hilo liliniumiza, iliumiza familia yangu na tukafika hatua hata kwenye familia ikaonekana kwamba kazi napaswa kuiacha, kwa hiyo ilinijeruhi binafsi.

Ikafika mahali sasa nikawa njiapanda, kwamba niache kazi ya utetezi au nifanye nini.

Nilikuwa napata simu nyingi sana, nina marafiki wa nje wengi, hawa wakawa wananiambia kama hali ni mbaya Tanzania, basi njoo huku.

Lakini unajikuta uko kwenye mtanzuko mkubwa wa nini cha kufanya. Je, nikimbie nchi? Nitaonekana nimekimbia vita. Au nibaki tu? Nikibaki huku nako familia wananung'unika kwamba unaweza kutuletea shida.

Kwa hiyo ni kipindi kigumu ambacho unajikuta katika hali ngumu. Mimi pia nilipata misukosuko mingi, nilikuwa ninakamatwa, niliitwa polisi mara kadhaa na wanakuja kunikagua pia mali zangu.

Bahati nzuri mimi pamoja na taasisi yangu, hawakuweza kukuta kitu chochote na polisi wenyewe baadaye wale waliokuwa wakifanya kazi, walisema kwa kweli sisi tumenawa mikono.

Hata hatua ya Rais Samia kuingia madarakani, kilinikuta bado natafakari nini cha kufanya, kumbuka marehemu (Rais Magufuli) ameondoka, akaunti zetu zimefungwa hatufanyi kazi, tuko kwenye mtanzuko.

Unapigiwa simu huku na huku, njoo njoo kwa hiyo niseme tu kwamba kitendo cha Rais Samia kuingia madarakani au cha Magufuli kufariki, ndiyo kilikuja kuondoa utata wa hatma yangu kwenye kazi hii. Kwa sababu kama ingeendelea, ninaamini ningekuwa tayari niko Segerea (gerezani) au wameniuu au ningeshakimbia nchi.

Kimsingi, pamoja na mashinikizo mengi, nisingeweza kuacha kazi hii, hata iweje nisingeweza kubadilisha kazi yangu hii, ni kazi yangu ambayo nitaenda nayo hadi nakufa.

Mimi ni wakili ningeweza kufanya biashara za kiwakili na biashara hiyo ningefanya vizuri tu, lakini hii kazi nimeifanya tangu nikiwa chuo ni miaka 20 sasa, sioni kama kwa hii miaka yangu iliyobaki hapa duniani, nina sehemu nyingine ya kwenda.

Namshukuru Mungu sala zilinisaidia nilikuwa nasali, watoto wangu walikuwa wanashindwa kwenda shule kwa kukosa ada, watoto wakawa wanauliza kwani umefanya kosa gani?

Inafika mahala hata watoto wasipoelewa waweza wakahisi kuna kosa ulilolifanya, kwanini sasa hivi imekuwa hivi; kwanini umefungiwa akaunti; kwa hiyo maswali yanakuwa mengi kwa mtu ambaye siyo mwelewa sana.



Kenya

Raila anavuruga ama anajenga nchi?



Na Julius MKAMBI

KIONGOZI wa upinzania Kenya, Raila Odinga, (pichani), kwa mara nyingine tena, amedhibiti-sha kauli kwamba kwenye siasa hakuna marafiki wala maadui wa kudumu ila kinachoangaliwa zaidi ni maslahi maalum tu.

Hii ni baada ya Rais wa Kenya William Ruto kujumuisha viongozi wanne wa ngazi ya juu kutoka chama cha upinzani cha Orange Democratic Movement (ODM) kinachoongozwa na Raila kwenye baraza lake la mawaziri.

Hatua hiyo ya Rais Ruto kuwa na mawaziri kutoka ODM, inaonyesha Raila amefanikiwa kujipenyeza serikalini.

Hii siyo mara ya kwanza kwa Raila kujipenyeza serikalini, kwani amewahi kufanya hivyo kwa serikali za awamu tatu zilizopita akianza na Rais Daniel arap Moi, kisha Mwai Kibaki, akafuata Uhuru Kenyatta na sasa Rais Ruto.

Dalili za Raila kuingia ndani ya serikali zilianza kujitokeza alipolazimika kuanusha kauli aliyotoa siku chache tu baada ya kukutana na Rais Ruto kwenye hafa ya kutia saini mchakato wa kuunda kamati itakayosaka makamishna wapya wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC).

Hatua hiyo ya Raila kuruhusu kuingia ndani

ya serikali ya Rais Ruto kunatishia kumeguka kwa muungano wa vyama vya upinzani chini ya mwavuli wa Azimio la Umoja huku ikiwa imebaki miaka mitatu Kenya kwenda kwenye uchaguzi mkuu.

Kitendo cha Raila kutoa kauli mbili zinazokinzana, inafuatia 'presha' ya vijana wa Gen Z ambao wamekuwa wakihamasishana kupitia mitandao ya kijamii kufanya maandamano ya amani kushinikiza uwajibikaji wa serikali.

Rais Ruto mara kadhaa amewataka Gen Z kusitisha maandamano ambayo yamegeuka vurugu na kusababisha baadhi ya waandamanaji kupoteza maisha na mali kuharibiwa.

Raila alipoonekana hadharani na Ruto, aliwaomba vijana kusitisha maandamano na kushiriki mazungumzo ya kitaifa yaliyoitishwa na Rais Ruto yenye lengo la kujadili ili kupata suluhu ya changamoto zinazozikabili taifa.

Hata hivyo, kauli ya mazungumzo ya kitaifa ilipingwa na vijana wa Gen Z wakisitiza wanachotaka ni Rais Ruto kutekeleza hoja walizowasilisha na kwamba mazungumzo aina hiyo yameshafanyika mara nyingi, lakini ripoti zake hazifanyiwi kazi.

Inaendelea Uk. 27



Raila anavuruga ama anajenga nchi?

Inatoka Uk. 26

Kama hiyo haitoshi, Gen Z ambao wameji-tambulisha kwamba hawana kiongozi, walisema Raila hana mamlaka kuwaambia wasitishe maandamano au kushiriki kwenye meza ya mazungumzo kwa sababu yeye siyo kiongozi wao.

Msimamo kama huo wa Gen Z pia unashikiliwa na viongozi wengine wa Azimio la Umoja wakiongozwa na Kalonzo Musyoka, Martha Karua, Eugene Wamalwa na Jeremiah Kioni, wakisisitiza upinzani haupo tayari kushiriki mazungumzo ya kitaifa.

Presha hii ya vijana wa Gen Z na viongozi wengine wa upinzani, ulisababisha Raila kubadili kauli yake na kutoa masharti anayopaswa kutekeleza Rais Ruto ili washiriki kwenye meza ya mazungumzo.

Swali ni je, nini kimesababisha Raila kutokuwa na msimamo? Je, ameshikwa 'mateka' na Rais Ruto? Au anajaribu kuwa mpatanishi kati ya Ruto na Gen Z ili kufungua milango ya mazungumzo akiamini ndiyo njia sahihi ya kuleta taifa pamoja?

Na je, itakuwa ni Raia, waziri mkuu huyo wa zamani anapokea shinikizo kutoka kwa baadhi ya wanachama wa ODM?

Rais Ruto alipovunja baraza zima la mawaziri siku chache baada ya kukataa kuweka saina Muswada wa Fedha 2024, alisema baraza jipya la mawaziri litakuwa pana akiwa na maana kuwepo kwa upinzani, hivyo kudokeza kuunda serikali ya mseto.

Ni jambo ambalo Kalonzo aliyewahi kuwa makamu wa rais alisema Azimio la Umoja hawatakubali kujiunga kwenye baraza la mawaziri la Ruto.

Dalili za Rais Ruto kuunda serikali ya mseto zilianza kujitokeza alipotangaza awamu ya kwanza ya mawaziri wapya 11 na ikasemekana awamu ya pili itajumuisha baadhi ya viongozi wa upinzani hususan kutoka ODM ambao wamependekezwa na Raila baada ya Ruto kumuahidi nafasi tano.

Katika kile kinachoonekana kudhibitisha hilo, moja wa wanachama wa ODM ambaye ni Mbunge wa Homabay Mjini, Peter Kaluma, alifichua bungeni kwamba yapo makubaliano kati ya

ODM na serikali anayoongoza Rais Ruto kuwajumuisha baadhi ya wanachama wa chama hicho katika nyadhifa zilizosalia za baraza la mawaziri.

Mbunge huyo alidokeza kwamba Raila alifanya mapatano na Ruto ili kupeleka orodha yake ya majina kwa ajili ya kuzingatiwa katika jitihada za kuunda serikali ya umoja wa kitaifa.

Hata hivyo, Katibu Mkuu wa ODM, Edwin Sifuna, katika taarifa alisema chama hakipo kwenye majadiliano kuhusu makubaliano yoyote au kushawishi uteuzi na serikali ya Rais Ruto.

Gavana wa Kaunti ya Siaya na moja wa wanasiasa wakongwe ndani ya ODM, James Orendo, akiongeza kwamba mwanachama yeyote wa chama hicho atakayeteuliwa uwaziri, atajiunga kwa utashi wake binafsi na siyo baraka za chama.

Kauli ya Orendo ilionekana kumkera Mbunge wa Kuteuliwa ambaye pia ni Mwenyekiti wa ODM, John Badi, aliyeyunga mkono mazungumzo na hata kuundwa kwa serikali ya mseto akisema ndiyo njia pekee ya kutatua changamoto zinazokabili taifa.

"Huwezi kutuambia kwamba hatuwezi kufanya mazungumzo, kwamba hatuwezi kuzungumza na Ruto na kwamba hatuwezi kukubaliana kama Wakenya. Je, ni nini mbadala?" Alihoji Mbadi ambaye ameteulia waziri wa fedha kwenye awamu ya pili ya baraza la mawaziri lililotajwa na Rais Ruto.

Wengine kutoka ODM walioteuliwa mawaziri na wadhifa wao kwenye mabano wakisubiri kupigwa msasa na Bunge ni manaibu wawili viongozi wa ODM, Wycliffe Oparanya (Mashirika na Biashara Ndogo), Hassan Ali Joho (Madini) na kiongozi wa wachache Bunge la Taifa, Opiyo Wandayi (Nishati na Mafuta).



Rais wa Kenya, William Ruto



Makala

Biashara ya hewa ukaa, mkondo mpya wa ukoloni



hewa ya ukaa

Na Mwandishi Wetu

NCHI kadhaa za Afrika “zinarukaruka kwa furaha” kuwa sasa zina uwezo wa kupata mabilioni ya dola za Marekani kupitia biashara ya hewa ukaa.

Lakini kimsingi wanachofurahia ni kifo chao – kwa sasa na vizazi vijavyo.

Iko hivi; nchi zilizoendelea zitakuwa zinatoa fedha (kama fidia) kwa nchi masikini ambazo zin-aendesha miradi ya kimazingira inayosaidia kupunguza kiwango cha hewa ya ukaa angani.

Yaani nchi tajiri zitaruhusiwa kuendelea na shughuli zao zinazozalisha kiasi kikubwa cha hewa na ukaa kama kawaida, lakini ili kuzuia hewa hiyo isiendeleo kuhatarisha maisha duniani, basi watatumia sehemu ya faida wanayoipata kutokana na shughuli zao kuzilipa nchi masikini ambazo zina miradi inayosaidia kupunguza hewa ukaa angani.

Maana yake ni kuwa nchi zilizoendelea zitaachwa ziendeleo kuzalisha hewa ya ukaa na nchi masikini zitakuwa zinalipwa ili kusafisha hewa

hiyo chafu inayozalishwa na nchi tajiri.

Lakini, ili nchi masikini ziweza kufaidi fedha hizo za biashara ya hewa ya ukaa, zinapaswa kutimiza vigezo na masharti kadhaa.

Vigezo na masharti hayo vinapangwa na nchi tajiri!

Tena ili nchi masikini ziweze kupata fedha hizo za biashara ya hewa ya ukaa, inabidi miradi yao ifanyiwe tathmini kuona kama inakidhi masharti na vigezo vilivyowekwa na wao.

Tathmini hiyo inafanwya na taasisi chache duniani ambazo zote zimeanzishwa, zinaendeshwa na zipo kwenye nchi tajiri.

Lakini, nchi masikini zinashangilia mpango huu kwa sababu zenyewe zinafikiria tu zile dola watakazopata, bila kujiuliza ni nini kinatokea kwenye hali hewa wakati nchi tajiri zinapoachwa ziendeleo kuzalisha hewa ya ukaa?

TFS yatoa neno

Hii siyo hali inayopaswa kuachwa iendeleo hivi-hivi. Kama hali itaachwa iendeleo itakuwa ni ndoto kwa dunia kupunguza ongezeko la joto duniani kwa sababu hewa ya ukaa itaendelea kuzalishwa.

Hivyo, jambo la muhimu ni kuhakikisha kuwa kiwango cha hewa ya ukaa kinachozalishwa kinapunguzwa na upunguzwaji wake usitokane na miradi katika nchi masikini, bali kupunguzwa kwa shughuli zinazozalisha hewa ya ukaa katika nchi tajiri kama ambavyo Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Huduma za Misituni nchini (TFS), Prof Dosantos Silayo alivyodokeza hivi karibuni.

“Biashara hii (ya hewa ya ukaa) inapaswa kufanyika kwa namna ambayo itafanikisha lengo lake kuu - la kupunguza kiwango cha hewa ya ukaa inayozalishwa...”

“Biashara inapaswa kuhakikisha kila upande unanufaika na maslahi ya kila upande yanazingatiwa,” anasema Prof Silayo.

Amesisitiza kuwa biashara hiyo haitakuwa na maana iwapo inazifanya baadhi ya nchi ziendeleo kuzalisha hewa ya ukaa, huku nyingine zikitumika kama vyombo vya kusafisha hewa hiyo inayozalishwa kwa wingi.

Dola zamwagwa Tanzania

Prof. Silayo anayasema hayo wakati ambao Tanzania nayo ni moja ya nchi ambazo tayari



Biashara ya hewa ukaa

Inatoka Uk. 28

zimeshaanza kunufaika na biashara hiyo.

Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulikia Mazingira, iliwahi kunukuliwa hivi karibuni ikieleza kuwa Tanzania inajipanga kuingiza kiasi cha dola bilioni moja kupitia biashara ya hewa ya ukaa.

Akizungumza kuhusu hillo, aliyekuwa waziri anayeshughulikia mazingira, Dkt. Suleiman Jafo alisema tayari miradi 39 yenye sifa za kupata fidia kupitia biashara ya hewa ya ukaa imeshasajiliwa huku miradi 12 kati yake ikiwa imepatiwa kibali cha kuendelea.

Akieleza uwezekano wa Tanzania kuanza kufaidi dola hizo, Jafo alieleza kuwa Wilaya ya Tanganyika inatarajiwa kupokea kiasi cha dola milioni 1.6 (shilingi bilioni 1.4 wakati wilaya za Mbulu na Kiteto zikiwa zimeshapokea dola milioni 2.1 (shilingi bilioni 4.8).

“Hii inaonyesha kuwa Tanzania ina fursa nzuri ya kutengeneza fedha kupitia biashara ya hewa ya ukaa,” alisisitiza Dkt. Jafo.

Hata hivyo, wakati Jafo akijinasibu kuwa nchi ipo tayari kwa biashara hiyo, hakuna ushahidi wa kitakwimu unaonyesha hivyo.

Mathalan, hadi hivi sasa hakuna takwimu zozote zinazoonyesha Tanzania ina uwezo gani wa kupunguza kiwango cha hewa ya ukaa wala hakuna

takwimu zinazoonyesha Tanzania imepunguza kiasi gani cha hewa ya ukaa licha ya kuanza kupokea mabilioni hayo ya fedha.

Kuhusu hilo, Prof. Silayo anasisitiza kuwa iwapo dunia inataka kuondokana na tishio la kuongeza kwa joto, basi kinachopaswa kufanyika ni kuhakikisha kuwa uzalishaji wa hewa ya ukaa unapunguzwa hadi viwango vilivyokubaliwa.

Alibainisha kuwa mtindo wa kuziacha baadhi ya nchi ziendeleo kuzalisha hewa hiyo hatari, huku nchi nyingine zikitumika kama chujio la kuiondoa, hautafanikiwa kwa sababu hakuna uhakika kuwa kiasi cha hewa kitakachoondolewa kupitia miradi hiyo, kitaendana na hewa iliyozalishwa.

Afrika, licha ya kuzalisha kiasi kidogo cha hewa ya ukaa, lakini ndilo bara linaloathirika zaidi kwa majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuwepo ongezeko la joto duniani.

Majanga kama vile vimbunga, mafuriko, ukame, kuongezeka kwa kina cha bahari, mvua zisizo na uhakika, ni kati ya mambo yanayoandama Afrika katika miaka ya hivi karibuni.

Kwa kiasi kikubwa mambo haya yote yanatokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Uzalishaji vs upunguzaji

Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, mwaka 2019 dunia ilizalisha tani milioni 48 za hewa ya ukaa, huku kiasi kikubwa cha hewa hiyo kikizalishwa na nchi zilizoendelea na zile zenye idadi kubwa ya watu.

Kwa wastani, kila mtu anazalisha takribani tani 6.2 za hewa ya ukaa kwa mwaka, lakini kuna baadhi ya nchi ambazo zinazalisha mara tatu ya wastani huu.

Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia kiasi cha uzalishaji wa hewa ya ukaa katika nchi zilizoendelea, ni mara mbili zaidi (tani 9.9 ya wastani wa dunia wa tani 4.6), huku nchi zinazoendelea zikizalisha wastani wa tani 1.7 ikiwa ni nusu ya wastani wa dunia na nchi masikini, zikizalisha kiasi kidogo sana cha wastani wa tani 0.3.

Nchi zinazotajwa kuzalisha hewa ya ukaa kwa wingi ni China (asilimia 30) na Marekani (karibu asilimia 14).

Hata hivyo, ukipima uzalishaji wa hewa ya ukaa kwa wastani wa idadi ya watu, nchi zinazozalisha mafuta za Qatar, Bahrain na Kuwait ndizo zinashika nafasi ya juu.

Makala

Tibaijuka akemea ‘uchawa,’ ni angamizo

Arodia PETER

TABIA ya vijana kuwa “chawa” wa viongozi na matajiri, haina mwisho mwema kwani inadumaza na kuua nguvu kazi ya taifa.

Uchawa ni tabia iliyozuka siku za karibuni, ambapo vijana hugeuka kuwa wapambe na “waimba mapambio” kwa wenye fedha ama madaraka bila uhalisia wa kile wanachosifia.

Profesa Anna Tibaijuka ambaye amewahi kuwa Mbunge wa Muleba Kusini na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, amewaonya vijana kuwa tabia hiyo inawamaliza na kwamba waendelea kuwa “vijana wa hovy” kama hawataacha tabia hiyo.

Ameliambia Pambazuko kuwa matajiri na wanasiasa wanaowafanya vijana kuwa ‘chawa’ wanajenga mazingira ya vijana kutothamini kazi, na kwa kudanganywa kwa senti kidogo.

“Jambo la uchawa linawadumaza vijana na kuwafanya washindwe kujitambua na kuacha kuwa na ndoto ya kujitegemea, ni tabia mbaya sana,” amesema Profesa huyo.

Amesema anashangaa kizazi cha vijana wa sasa kushindwa kuwa na ndoto kubwa na badala yake wanabaki kuwa “watu wa kujikomba kwa wanasiasa na wenye fedha.”

“Kizazi cha Mwalimu Nyerere (Julius – Rais wa kwanza ka Tanzania), ambacho mimi ni miongoni mwao, kilifundisha watu kufanyakazi na kujitegemea na si kuwa kama kupe, kunyonya damu bila kufanya kazi...”

“Siku hizi kuna mambo ya uchawa, huwezi kuchangia chochote kwenye jamii ukiwa kwenye uchawa, chawa hatafuti cha kwake, kazi ya chawa anafyonza damu za wengine...”

“Lakini vijana hawataki kuwa ‘machawa,’ ila wabaya ni wale wanaowafanya vijana kuwa ‘machawa.’ Mimi nimelelewa na Mwalimu Nyerere, tuliambiwa usiwe kupe, ujitegemee, kwa hiyo katika kizazi changu, sisi tunasimamia msimamo huo,” alisema Profesa Tibaijuka.

Tibaijuka aongezewa udaktari

Profesa Tibaijuka ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji (mstaafu) wa Shirika la Makazi Duniani

(UN-Habitat) juzi alitunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari (Doctor of Philosophy in Humanities) kutoka Chuo cha United Graduate College and Seminary International cha nchini Marekani, alisema atahakikisha mchango wa heshima hiyo unaonekana kwa jamii.

Mshindi wetu ni Janeth Jovin



Pambazuko limepokea tafsiri 321 kutoka kwa wasomaji wake, na baada ya kuzipitia, zimepatikana bora zaidi tatu kutoka kwa; Wakili Msomi – Igosha Novatus; Janeth Jovin na Masaga Mlyasele na aliyeibuka kinara ni Janeth ambaye anapokea Shilingi 10,000.

Tafsiri ya Janeth: Watoto (ama wajukuu) wanasubiria chakula, mpishi hakuwa na kitu cha kuwapikia, lakini anajiziba ili wasimuone kwamba anapika moyo wake ili wao wale. Huu ni upendo wa kinama, ambao wako radhi kutoa kila kitu ili vijana wao waendelee kuishi.

Pambazuko linawapongeza wote walioshiriki na kuwaomba waendelee kusoma gazeti na kuchemsha bongo kupitia ukurasa wa 5 - Mhariri.



Tamu, chungu ya ndugu wa tumbo moja kuolewa na mume mmoja

KATIKA utangulizi wiki iliyopita nilidokeza kuwa tutaanza kuangalia suala la ndoa. Hili ni jambo pana na lina mengi ya kufuatilia.

Hapa nchini masuala ya ndoa yanaongozwa kisheria. Sheria inatambua ndoa za aina mbalimbali; ndoa za kidini au za kimila na za kiserikali.

Lakini chini ya taratibu hizo za kidini, kimi-la na kisheria, hatimaye watu wawili; mume na mke, wanaishi pamoja wakiwa wenza.

Wengi tunafahamu kuwa msingi wa ndoa za kidini ni amri ya Mungu inayowataka watu kui-shi pamoja, mke na mume baada ya kuoana.

Lakini kuna tofauti kuhusu idadi ya wake ambao mtu anapaswa kuwa nao. Katika dini ya Kiislamu, mwanaume anaruhusiwa kuoa hadi wanawake wanne, wakati kwenye Ukristo, mwanaume haruhusiwi kuoa zaidi ya mwanamke mmoja.

Suala hili la ndoa za Kikristo, linaonekana kuwa na utata kama ambavyo mmoja wa maas-kofu maarufu nchini, Anthony Lusekelo 'Mzee wa Upako', alivyodokeza wakati akihojiwa na ki-tuo kimoja na habari hivi karibuni.

Katika maoni yake, Askofu Lusekelo alibain-isha kuwa maandiko katika Biblia yanaonyesha kuwa zamani mababu walikuwa na zaidi ya mke mmoja, ingawa siku hizi sheria za dini zinataka mwanaume aoe mwanamke mmoja tu.

Lakini kama nilivyosema awali, iwe ni mke mmoja au wake wengi, hatimaye watu hawa wa-naishi pamoja, na hapo ndipo suala la uhusiano linapokuja.

Ukiacha suala la idadi ya wake wa kuoa, katika makabila kadhaa nchini, suala la mwa-namume mmoja kuona ndugu wa tumbo moja ni ka lawaida.

Jambo hilo lina faida na hasara zake. Kwa

upande mmoja linatumika kama njia ya kuim-arisha upendo ndani ya familia.

Katika baadhi ya nyakati, mwanaume huoa mdogo wa mke wake kama dada huyo amesh-indwa kupata watoto.

Hivyo mdogo wake analetwa ili azae na mwanaume huyo kama njia ya 'kuendelea ukoo.'

Hapa, kwa sababu mara nyingi anayechagua ndugu wa kuolewa na mume wake ni dada, basi utakuta ni nadra kwa wawili hao kugombana.

Ipo mifano mingi katika makabila kadhaa nchini ambako utamaduni huu unafanyika.

Safu hii imezungumza na watu kadhaa kuto-ka Mkoa ni Kagera ambao wamethibitisha kuwa hilo ni suala la kawaida kwa baadhi ya koo huko kwao.

Inaaminika kuwa iwapo mwanaume ataona mke ambaye hana unasaba na mke aliyenaye, basi watoto wa mke wa kwanza watapata shida wakiishi na mama wa kambo iwapo mama yao atafariki dunia.

Lakini kama atakayeolewa ni dada wa tum-bo moja na yule mke mkubwa, basi ulinzi na mapenzi kwa watoto yatakuwa yamehakikishwa endapo mama yao mzazi atafariki kwa sababu watalelewa na mama yao mdogo.

Itaendelea...

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0754 88 67 49.



Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles

Namna mwanaume anavyoweza kuwa sahihi kimavazi

KUVAA nguo bila mpangilio kunapoteza utanashati wa mhusika pasipo kujali kuwa nguo hizo ni za gharama kubwa kwa kiasi gani.

Katika kundi hili, baadhi ya wanaume wamekuwa wakivaa nguo za gharama lakini hawaonekani kuwa watanashati kwa sababu tu hawazipangilii vyema zikaonekana katika muonekano wa kipekee na unaobeba haiba nzima.

Leo katika ukurasa huu wa mitindo, nimekuwekea vitu vitakavyokusaidia kuangalia namna bora ya kupangilia muonekano wako na kukufanya uwe mtanashati.

* Kama ni mvaaji wa suti; jita-hidi kuvaa ile inayokutosha vyema, iendane na mwili wako.

* Vaa saa nzuri; kama una pesa jita-hidi kuwa na saa ya gharama inayovutia. Saa hubeba mwonekano wa mtu na kukufanya wa tofauti kwa wanaokutazama.

* Usiwe mwoga wa kujaribu rangi; si kila rangi itakufaa lakini kuna rangi ambazo unaweza kuvaa na zikakuongezea utanashati wako. Usishindwe kuvaa rangi fulani kwa kuhofia watu, jaribu kuona mwenyewe inavyokukaa lakini pia si kila rangi unaweza kuvaa hususani kwenye mashati na suruali.

* Ipe thamani suruali yako ya jinzi na si kuvaa kimazoea. Angalia tisheti bora au shati na kiatu kitakachoibeba jinzi yako kwa usahihi.

* Mwanaume kujitazama kwenye kioo si dhambi, pitia muonekano wako kabla hujaondoka nyumbani.

* Nguo za ndani imara zitakufanya ujisikie vizuri.

* Kiatu bora kinakamilisha utanashati wa mwanaume, wapo baadhi ya watu wanapokutana na mtu huanza kwa kuangalia miguuni, yaani huko ndio hubeba mwonekano mzima.

* Mwanaume punguza urembo wa mikononi, ukivaa 'bracelet' moja inatosha.



Hudumia uso wako

USO ni sehemu muhimu kwani ndio mapokeo ya mwonekano wa mtu. Uso unatoa taarifa haraka za mtu ambaye ana hasira au furaha.

Vivyo hivyo, uso ukiwa mchafu, una chunusi au hautunzwi vyema huonesha kukosa nuru.

Fanya haya kutunza uso

Tumia vifaa vya usoni wakati wa kunawa uso wako kama subuni ya usoni nk. Wataalamu wanashauri kuepuka sabuni za vipande hasa zile za kufulia...

* Fanya scrub ya uso angalau mara mbili kwa mwezi.

* Fanya mazoezi ya mwili ili kutoa jasho litakalotoa taka zisizo-hitajika mwilini.

* Kunywa maji ya kutosha ambayo yatasaidia kuifanya ngozi yako kunawili na si kukauka.

* Inashauriwa kutumia maji ya uvuguvugu kila unaponawa uso wako ili kuzibua matundu na kisha malizia kwa maji ya baridi kuziba matundu.

* Tumia bidhaa kulingana na uso wako, kama ni wa mafuta jiepushe kutumia vitu vya kuongeza mafuta. * uso wa mafuta unaweza kutumia ute wa yai na maji ya limao kwa kupakaa ndani ya robo saa kisha nawa maji uvuguvugu.



Afcon



Bongo Fleva ijipange kung'ara Pamoja Afcon 2027

Na John MARWA

ALIYE kando haangukiwi mti. Hii methali ya Kiswahili yenye maana kwamba, aliyejitenga na mabaya, kamwe hayampati.

Tanzania, Kenya na Uganda ziko mbioni kuhakikisha zinaandika historia ya kuandaa mashindano ya Mataifa ya Afrika; "Pamoja Afcon 2027," ambapo maandalizi yamepamba moto kila nchi ikiwa katika maandalizi ya kufanikisha mashindano hayo makubwa Afrika.

Ni wazi miongoni mwa vitu ambavyo huambatana na mchezo wa soka ni burudani ya muziki ambapo imekuwa ikishuhudiwa katika mashindano mbalimbali ama fainali za mchezo huo, wanamuziki hupata nafasi ya kutumbuiza ama hata kutunga tungo za shindano husika.

Tunapoelekea Pamoja Afcon 2027, basi niwa-kumbushe wasanii wa Tanzania, Kenya na Uganda, kuhakikisha kuwa wasiingie vitani bila silaha nje ya dakika 90 za kandanda, kwa kuhakikisha wanauza muziki wa Bongo Fleva katika jukwaa hili kubwa la soka Afrika.

Siyo kwamba wasanii hawajui nini wanap-swa kukifanya, la hashu! Bali acha nitie pilipili kwenye kidonda ili maumivu yasiwe ya kwetu pekee, ila hata watakaokuja nao waonje ladha adhimu ya Bongo Fleva.

Hakuna jambo gumu ama lisilowezezana kuona wasanii kutoka ukanda huu wakitawala mashindano hayo kwa kuwa na tungo za shindano, lakini pia kupata fursa ya kutumbuiza katika kusherehesha za Pamoja Afcon 2027.

Ikumbukwe kuwa Mfalme wa Bongo Fleva, Ally Kiba 'King Kiba' alitumbuiza katika ufun-guzi wa 'African Football League (AFL)' yaliyoz-induliwa mwaka jana katika Dimba la Benjamin Mkapa, ambapo Timu ya Simba alikipepeti na Al

Ahly ya Misri, mbele ya viongozi wakubwa wa mpira wa miguu duniani.


Basi ni wakati sasa kwa Tanzania, Kenya na Uganda kuumiza vichwa kwani ni muda wa 'Enda na uchao, usiende na uchwao,' – kwamba kumeshakucha na tayari jua la-chomoza pwani ya Afrika mashariki, na sasa ni wasaa wa kuifanya Pamoja Afcon 2027 kuwa ya kwetu kivyetu vyetu wana Bongo Fleva.

Kama babu zetu walivyotuasa kuwa 'fimbo ya mnyonge, ni umoja,' basi ni wakati ambao umoja utatupa ushindi wa kuichukua Afcon na kuificha Kigoma kwao Ally Kiba na Diamond, ama kwa kina Phina Usukumani ni wakati wa Nyan-shisiki, Otile Brown, Sauti Soul kuitembe-za mitaa yote ya Nairobi na ni wakati am-bao Keneth Mugabi ama Silver Kyagulanyi walete swaga za Kampala ndani ya 'Bongo Fleva Pamoja Afcon 2027'.

Basi kila nchi ndani ya Afrika Mashari-ki, iumize vichwa kwa heshima ya Baba wa Taifa aliyelala pale Mwitongo Butiama, Hayati Julius Kambarage Nyerere, pale Kenya, Jomo Kenyatta na pale Uganda, Milton Obote.



Alikiba akitumbuiza kwenye ufun-guzi wa AFL.



Kichupa

cha Marioo
chawakosha JK,
Mwinyi, Majaliwa



Dar Es Salaam, TANZANIA

KICHUPA cha msanii wa Bongo Flewa, Marioo, kina-chokwenda kwa jina la 'Hakuna Matata' kimewakosha Rais mstaafu Jakaya Kikwete, Rais wa Zanzibar, Hussein Ali Mwinyi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Ngoma hiyo iliyo mpya ambayo ipo katika miondoko ya amapiano ameitambulisha kwa mtindo wa kipekee wa kuwajumuisha viongozi wakuu wa nchi kuitazama kabla haijatokea rasmi.

Tukio hilo limefanyikia Ikulu ya Zanzibar ambapo

aliambatana na muongozaji wa video hiyo, Kenny, pamoja na meneja wake.

Ikumbukwe pia siku za karibuni msanii huyo alipata fursa ya kutumbuiza kwenye harusi ya mtoto wa Rais wa Zanzibar, Jamila Mwinyi, ndoa iliyofanyika hivi karibuni Zanzibar na kutikisa nchi.

Video hiyo imeachiwa siku ya Alhamisi na kupokelewa vizuri na mashabiki wa kazi zake kwani hadi sasa imefanikiwa kufikisha jumla ya watazamaji laki 4 ikiwa ni masaa machache tangu kuachiwa kwake kwenye mtandao wa YouTube.

Ditto aangukia pua kesi ya Bil. 6/-

Na Mwandishi WETU


MSANII wa bongo flewa Lameck Ditto, maarufu kama Ditto wiki hii ameangukia pua kwenye kesi alioifungua dhidi ya Kampuni ya Multichoice Tanzania kwa kupitia Kituo cha Televisheni cha Dstv, aki-watuhumu kutumia 'second version' ya wimbo wake wa 'Nchi Yangu' badala ya 'Original Version'.

Ditto alifungua madai hayo kwenye Mahakama kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es salaam mwaka 2020, akidai kwamba 'second version' ya wimbo huo ilitumika kwenye Tamasha la Urithi Festival.

Ditto ameshindwa kesi hiyo ya madai ambapo alikuwa akiomba Mahakama iamura Multichoice Tanzania imlpe fidia ya Sh. bilioni 6 kwa kutumia wimbo wa "Nchi Yangu".

Katika kesi ya msingi, Ditto alikuwa akilalamikia Dstv kuwa walitumia wimbo huo katika kampeni za Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, ambapo aliomba mahakama iamura Dstv imlpe milioni 200 kama sehemu ya fidia kutokana na madhara aliyopata. Pia, katika kesi hiyo, Ditto ali-peleka mashahidi watano na Dstv ilikuwa na mashahidi wawili, Astrid Mapunda na Johnson Mshana wakiongozwa na mawakili, Simon Lyimo na Thomas Mathias.

Kwa upande wa Ditto, baadhi ya mashahidi wake walikuwa ni mtayarishaji wa wimbo huo, Emmanuel Maungu (Emma the boy), meneja wake, Rodney Rugambo na Angela Karashani wakiongozwa na mawakili, Ally Hamza na Elizabeth Mlemeta



Calafiori

Beki wa kati kutoka Bologna, Riccardo Calafiori amejunga na klabu ya Arsenal kwa ada ya pauni milioni 40 kwa kandarasi ya miaka mitano.

Neves



Klabu ya Paris Saint Germain (PSG), imeanza mazungumzo na kiungo, João Neves kutoka Benfica, kiungo huyo anataka kwenenda kucheza PSG msimu ujao.

Ilenikhena

Klabu ya Monaco imemsaajili mshambuliaji, George Ilenikhena, kutoka klabu ya Royal Antwerp FC ya Ubelgiji kwa ada ya Euro milioni 20 kama sehemu ya uhamisho wake.



Tanzania itavuna nini Olimpiki 2024 Ufaransa?

Na Mwandishi WETU

MICHEZO ya Olimpiki kwa mwaka 2024, imeanza huko Paris, Ufaransa, huku Tanzania ikiwa na matarajio makubwa ya kupata medali kupitia wanamichezo saba wanaoiwakilisha.

Tanzania inashiriki michezo hiyo ya Olimpiki ya Paris 2024 kama sehemu ya juhudi zake za kuendeleza michezo na kukuza vipaji vya wanamichezo wake.

Hii ni nafasi nyingine kwa nchi kuonesha uwezo wake katika jukwaa la kimataifa.

Wanariadha wanne; Alphonse Simbu, Gabriel Geai, Magdalena Shauri na Jackline Sakiru – wote wakiwa wanakimbia mbio ndefu, ni miongoni mwa wawakilishi hao.

Pamoja na riadha Tanzania inawakilishwa pia na Andrew Mlugu ambaye anashiriki kwenye mchezo wa Judo. Pia kuna mabondia wawili.

Swali kubwa hapa kutoka kwa Watanzania ni moja tu; je, wanamichezo wake watawuna na kurejea na nini nyumbani?

Katika pambano la kwanza Mlugu anatazamiwa kushuka ulingoni leo akikabiliana na William Tai Tin wa Samoa.

Akizungumza na vyombo vya habari hivi karibuni, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Alfred Tandau, alionyesha matumaini yake kuwa wanamichezo hao watafanya vyeema katika michezo hiyo.

Alisema hilo linatokana na maandalizi yaliyofanyika, lakini pia

na ari ambayo wanamichezo hao wameonyesha kwa kuwa na shauku ya kupata mafanikio binafsi na nchi kwa jumla.

Kwa kawaida Serikali na TOC hufanya kazi kwa karibu na vilabu vya michezo na mashirika mbalimbali ili kuhakikisha wanamichezo wanaodhamiria kushiriki michezo ya Olimpiki wanapata mafunzo na vifaa vinavyohitajika.

Maandalizi haya yanahusisha kambi za mafunzo ndani na nje ya nchi ili kuboresha uwezo wa wanamichezo.

Hata hivyo, kama ilivyo kwa nchi nyhingi zinazoendelea, Tanzania hukumbana na changamoto za kifedha na vifaa vya kutosha kwa ajili ya kuandaa wanamichezo wake.

Ushiriki wa Tanzania katika Michezo ya Olimpiki ya Paris 2024 ni muhimu siyo tu kwa wanariadha binafsi, bali pia kwa taifa zima katika kukuza michezo na kuleta sifa kwa nchi.

Ufunguzi wa aina yake

Kupitia hafla ya ufunguzi wa michezo hiyo Ijumaa jioni Ufaransa ilipata fursa ya kuonyesha utamaduni wake kupitia muziki, mitindo na mambo mengine kadhaa.

Katika tukio la aina yake utambulisho wa nchi zinazoshiriki michezo hiyo ulifanyika katika mto mkubwa wa unaokatiza katika Jiji la Paris uitwao Seine.

Wanamuziki nguli duniani, Celine Dion, Lady Gaga na nyota wa muziki wa RnB, Aya Nakamura ni miongoni mwa wanamuziki mahiri waliotumbuiza.

MICHEZO

Jumatatu, Julai 29 - Agosti 4, 2024



Nahodha wa timu ya Yanga, Bakari Nondo Mwamnye-to akiwa amebeba Kombe la Toyota baada ya kuichapa timu ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini magoli 4-0 katika mchezo wa fainali uliochezwa kwenye Uwanja wa Toyota mjini Bloemfontein jana. (Picha na Yanga)

Yanga hii, haipoi, haiboi

Na Mwandishi Wetu

TIMU ya Yanga ya moto na itaendelea kuzipa shida klabu pinzani kwa msimu huu kama ilivyokuwa kipindi kilichopita kwa mabingwa hao wa kihistoria.

Picha linaanza wameanza vizuri kwa kutwaa Kombe la Toyota baada ya kuwashushia kipigo kizito wenyeji, Kaizer Chiefs mabao 4-0 katika Uwanja wa Toyota mjini Bloemfontein nchini Afrika Kusini jana.

Mabao ya Yanga yamefungwa na mshambuliaji, Prince Dube Mpumelelo dakika ya 25, huku kiungo mshambuliaji, Stephane Aziz Ki akitupia mabao mawili, dakika ya 45 na 63 wakati bao la nne likifungwa na mshambuliaji mzawa, Clement Francis Mzize ambaye sasa anatumika kama winga, dakika

ya 57.

Baada ya mchezo huo, Aziz Ki alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mechi hiyo na kupewa mfano wa hundi huku Yanga wakikabidhiwa Kombe.

Yanga inakamilisha mechi zake za kirafiki katika ziara yake ya wiki mbili nchini Afrika Kusini.

Katika mashindano hayo kwenye mechi ya ufunguzi walipigwa 2-1 na klabu ya Augsburg ya Ujerumani baadaye walishinda 1-0 dhidi ya TS Galaxy mjini Mpumalanga.

Mabingwa hao wa Tanzania sasa wanatarajiwa kurejea nchini kwa ajili ya tamasha la Kilele cha Wiki ya Mwananchi Agosti 4 Uwanja wa Benjamin Mkapa Jijini Dar es Salaam.

Baada ya hapo watamenyana na Simba SC katiwa Nusu Fainali ya Ngao ya Jamii Agosti 8 Uwanja wa Mkapa.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

